# *Kushawishika Na Kisha Kuhusika*

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kabla tu hatujaenda mbali zaidi. Endelea na huo, Dada Anna Jeanne, tafadhali, na ndugu. Akishuka kutoka kwenye kilima alikuja Mgeni kwa watu siku moja. Akaangalia chini kwenye mandhari kwenye ku—kundi la watu aliokuwa amewaagiza kutoa pepo, kuponya wagonjwa, Naye akawakuta wameshindwa na ugonjwa wa kifafa.

Labda Yohana alikuwa akisema, "Hivi ndivyo tulivyolifanya huko Kapernaumu."

Huyo mwingine akasema, "Hivi ndivyo tulivyolifanya mahali pengine." Lakini halikuleta matokeo.

2 Ndipo baba ya huyo mtoto akaanglia, naye akaona Mtu akija. Akakimbia, akaanguka chini. Akasema, "Bwana, nilimleta mtoto wangu kwa wanafunzi Wako, nao wasingeweza kumponya." Kasema, "Waweza kumfanyia lolote?"

Akasema, "Ninaweza, ukiamini." Yuyo Huyo amekuwa pamoja nasi. Yuko pamoja nasi asubuhi ya leo. "Ninaweza, ukiamini." Um-hum.

3 Baba yetu wa Mbinguni, katika utakatifu wa ibada hii, tukijua kwamba Mungu tunayemwabudu si sa—sanamu, kama vile makafiri wangeichukua sanamu na kuisujudia, na ya mungu wa kuwaziwa, na kuamini kwamba sa—sauti ya kuwaziwa iliwajia, kwamba alijipumbaza akili akawa sanamu.

4 Ni jambo la kigeni jinsi gani kwa shetani kufanya jambo kama hilo, wakati kweli, Mungu ni Roho, kwamba haingii katika sanamu, bali Yeye huingia katika wanadamu walio hai na kunena Maneno Yake Mwenyewe kupitia kwa mtu huyo. Nasi ndio sura Zake zilizo hai, zilizoumbwa kwa mfano Wake, na kwa ajili ya kazi Yake, na kwa utukufu Wake.

5 Nasi tunawaona wagonjwa na wanaoteseka karibu nasi. Ndipo, Bwana, tu—tunaona tumezembea kazini. Kuna kitu fulani mahali fulani tunachohitaji, Bwana. Utupe asubuhi ya leo, sivyo, Baba? Nikiwa nimesimama, nikimsikia huyu ndugu mwenye neema akizungumza juu ya jambo hilo walilokuwa nalo miaka mingi iliyopita katika—katika mkutano huo wa Mtaa wa Azusa. Alikuwa ndiye mtu mdogo zaidi kule, akitaka kutambaa chini ya benchi.

6 Mungu, laiti ningaliona hilo likitokea tena, ambapo kila mtu, na watu hawaninii. . .wasiwe wakubwa, bali wawe

wadogo, wajinyenyekeze. Mungu, tutumie tena katika siku zetu. Tuna kuchochewa, na uanachama, na kadhalika. Lakini tu—tunamtaka Yesu. Tunakutaka Wewe, Roho tunayejua yuko hapa amekusanyika pamoja nasi asubuhi ya leo. Tunakutaka Wewe ndani yetu, Bwana. Tunataka sisi wenyewe tutoke. Tufanye tupu, Bwana, na utujaze na Uwepo Wako. Inyenyekeze mioyo yetu, nasi tutakusifu.

7 Sasa, tumekusanyika, Baba, kwa ushirika katika Neno. Wewe ni Neno. Nasi tunaomba ya kwamba utajigawa Mwenyewe miongoni mwetu asubuhi ya leo na kutufanya mmoja katika moyo, mmoja katika kusudi. Kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

8 Wakati mwingine ninaposikia shuhuda kama hizo nilizopata fursa ya kusikiliza kwa yapata dakika tano asubuhi ya leo, la—laiti ningaliweza tu kumwambia huyo ndugu arudi hapa, na kuniruhusu tu kuketi pale na kusikiliza jambo hilo. Mnaona? Anazungumzia jambo lile lile kabisa ninalotaka kuona likitukia tena, nataka, a-ha. Mtu huyo anasimulia tu yaliyokuwako, nami ninajaribu, kusema, “Hebu tuupate tena.” Sasa, jambo ndi—ndilo hilo tu.

9 Vema, kama ndugu yetu alivyosema, hakuna mtu anayeweza kuileta: inahitaji Mungu. Nasi hatuwezi kulifanya mpaka Mungu atufanyie. Hiyo ni kweli. Inahitaji Mungu. Hizo hapo shule zote, na wahudumu wote, na elimu zetu zote, na madhehebu yetu yote, na haidhuru ni kiasi gani tulipeana mikono na kujaribu kuingia katika umoja, na hilo—hilo lingekuwa sawa, hilo lingekuwa sawa, lakini inahitaji Mungu kuleta kitu kama hicho. Hicho pekee. Mungu hukileta.

10 Nataka kuninii . . . Hii ni shule ya Jumapili, na, loo, shule ya Jumapili kwa kawaida sihubiri zaidi ya saa tatu ama nne, na kwa hiyo mimi . . . Tuna muda mwingi asubuhi ya leo, na mimi—mimi ningependa tu kusema nimekuwa nikiwaangalia baadhi ya jamaa wa huko maskanini huku chini. Sipati nafasi ya kuwaona, nami, au, kuzungumza nao lakini ninaanza sasa asubuhi ya leo, kwa kuwa hii ni nuru tofauti, si nuru ya bandia, ni nuru kutoka kwa jua, ninaona baadhi ya marafiki zangu ambao mimi, kwa mara yangu ya kwanza ninaona, ninamwona Ndugu Welch Evans na mkewe wameketi kule nyuma, na familia, kutoka Tifton, Georgia. Kila wakati ninapozungumza huko maskanini mtu huyo huendesha gari safari ya maili elfu moja na mia tano, yeye na familia yake, kila Jumapili kusikia Injili. Ndugu Welch, laiti wewe na Dada Evans, familia hapo, mngesimama tu kwa dakika moja. Maili elfu moja na mia tano . . . Asanteni.

11 Ninakumbuka vizuri sana mara ya kwanza nilipomwona Ndugu Evans. Ndugu Mercier alisema, “Kuna mtu anayetaka kukutana nawe asubuhi.” Nilikuwa Philadelphia na . . .

ilipotokea, na nilipokuwa nikitoka kitandani nilimwona mtu huyo. Na kidogo yeye ni mwana-michezo, anapenda kuvua samaki. Nami nilimwona akikiuka sheria. Kwa hiyo asubuhi niliyokutana naye nilimwambia Meda kuhusu hilo.

Akasema, "Hungesema hivyo kwa mtu huyo mgeni."

Nikasema, "Nitajua yeye ni nini kwanza."

12 Kwa hiyo basi, baada ya kuzungumza naye, nikiona kwamba alikuwa muungwana kweli, nikasema, "Aisee, hivi majuzi tu ulikuwa ukirudi kutoka kwenye safari ya uvuvi, kama kwenye kinamasi. Ulikuwa na gunia zima lililojaa samaki, na ilikulazimu kuwaficha mara tatu, usije ukapatikana na mlinzi wa wanyama." Jamani.

Nikiangalia, kasema, "Naam, bwana. Mimi—mimi . . . " Ki—kile anacho- . . . kashangaa ningesema nini.

Nikasema, "Kuna ombi moja tu: Je, utanipeleka kuvua samaki huko?"

13 Ndugu yake alikuwa ameumwa na nyoka huko nyuma, ambaye alikuwa ni nyoka mchacharishaji wa ardhini. Sijui kama wanao hapa Louisiana au la. Naye ni maskini mnyama katili. Naye mvulana huyo, akalazwa hospitalini, yeye si Mkristo, kijana, mdogo kidogo kuliko Ndugu Evans hapa, naye ilimbidi kufungiwa gango mguuni mwake—akatembea kwa chuma, miezi kadhaa.

14 Na kwa hiyo, tukarudi mahali pale pale, mwajua, kwa namna fulani Bwana aliniambia, nirudi kule, basi ni—nikashika baadhi ya samaki wakubwa wazuri sana (Loo, jamani!), jamaa wakubwa mno. Nami nilikuwa na mmoja mkubwa aliyekuwa ameshikwa na ndoana, nilikuwa nikijaribu kumtoa (kwa kizibo nyukibambi, mwajua), na kwa hiyo, naye alikuwa mkubwa *hivi*, mdomo wake karibu namna *hiyo*, na hiyo nyukibambi ndogo mle ndani. Angesimama moja kwa moja kwa mkia wake (nyinyi wavuvi mnajua), naye angekirusha kitu hicho nje. Inabidi tu umshike. Usipomshika, unaking'oa, na kidogo ni vigumu. Alikuwa amekasirika, nami nikamrusha nyuma, na nilikuwa naye mara tatu au nne. Angekuwa samaki wa ratili kumi na mbili, kumi na nne.

15 Kwa hiyo Ndugu Evans aliniona na . . . Loo, yeye ni mvulana mzuri tu wa mashambani, mwajua; alikuwa amekunja miguu ya suruali yake, kwa sababu alikuwa amelowa maji. Na kwa hiyo akasema, "Lazima awe mzee Big Jim."

Nikasema, "Hapana shaka ndiye." Kwa hivyo nikaitupa tena, na—nami nikamshika mmoja.

Akasema, "Huyo ndiye."

Nikasema, "La, siye hasa." Ilikuwa ni samaki mkubwa mzuri.

16 Nasi tulibeba bastola ndogo kwenye nyonga zetu, kwa sababu ilikubidi kushambuliana na mamba mapitoni na—na nyoka wenye sumu kuingia mle, kinamasi tu, ekari elfu kumi na saba katika ranchi hii. Na imekuwa. . . Kizoa taka kilipitia humo, na hiyo. . . miaka iliyopita, na hapo ndipo tulipokuwa tukivua samaki.

17 Na kwa hiyo, ilitubidi kutembea majini na kila kitu ili tuingie mle, na mamba, nyoka, kwenye takataka tu. Na kwa hivyo, tungechukua ufito, na kuzunguka kote. Kama tungemwona nyo—nyoka mchacharishaji wa ardhini, tunampiga risasi tu, na kisha kutembea tu majini, mnaona, kuendelea mbele, maana angekuwa amelala juu ya yungiyungi, ama chochote kile, amejikunja, tayari kushambulia.

18 Kwa hiyo Ndugu Welch akasema, "Nitamwokota, samaki wako." Naye akaruka kutoka katika baadhi ya nyasi nyororo na laini pale. Basi alipofanya hivyo, nyoka mchacharishaji wa ardhini akamwuma, karibu tu, loo, yapata nusu maili kutoka mahali ambapo ndugu yake alikuwa amempata, akaumwa.

19 Vema, akaruka kutoka majini pale akiwa na matundu mawili mguuni mwake, mguu, juu tu, namna *hiyo*, ambapo jino la nyoka lilikuwa limeuma. Naye akasema mifupa yake ilikuwa ikiganda ndani yake.

20 Sasa, ikiwa umeona ukubwa wake, yeye ni mkubwa zaidi kuliko nilivyo mimi. Na ingenibidi kumbeba kama maili mbili mgongoni mwangu, nimtoe pale. Hilo lilinizidi. Nasi tulikuwa tumeketi pale, yeye akiushikilia, akiteseka.

Ndipo Bwana akazungumza tu nami, kataja Andiko: "Watakanyaga vichwa vya nyoka na nge; hakuna kitakachowapinga. . . kitakachowadhuru."

21 Nikasema, "Hebu kidogo, Ndugu Evans." Nikaweka mkono wangu mahali alipoumwa na huyo nyoka mguuni mwake. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, tuko katika hali ya hatari. Na imeandikwa, 'Waki-. . . wakishika nyoka, au wakikanyaga vichwa, haitawadhuru. Hiyo ilikuwa kwa ajili ya waaminio, naye ndugu huyu ni mwaminio. Nami ni mwaminio. Nasi tunaomba rehema Zako."

22 Kwa namna fulani akasimama, "Shiish, hah!" akipumua na kuteseka jinsi alivyokuwa. Nami nilifikiri alikuwa, kwa heshima tu ya maombi. Nilipomaliza, alikuwa akicheka. Kasema, "Maumivu yote yamekwisha." Akavaa tu viatu vyake na kuendelea.

23 Mnamo saa tano usiku huo, walikuwa huko nje wakipiga picha tulipofika mahali tulipokuwa tunakaa, motelini, tulirudi kutoka kwenye hiyo ranchi. Ndugu yake ana duka la chambo wakati huo, ng'ambo tu ya barabara. Vema, walikuwa pale wakipiga picha za safu hizi kubwa za—za samaki hawa wakubwa wa mdomo. Na kwa hiyo akasema. . .

24 Tulipokuwa—tulipokuwa tumesimama pale hoja ilitokea kuhusu kuumwa na nyoka. Ndugu yake akasema, "Ni vizuri kuwa wa kidini, lakini sio vizuri kuwa mjinga." Akasema—akasema, "Afadhali upate usaidizi wa matibabu sasa hivi." Mnaona? kwa sababu alikuwa na gango kutokana na namna hiyo hiyo ya kuumwa.

25 Akasema, "Niliumwa leo asubuhi yapata saa tano. Hii ni saa tano alasiri ya leo. Mungu ambaye angeweza kunilinda umbali huu, anaweza kunilinda kote katika safari iliyosalia." Kwa hiyo haya basi. Mnaona, Yeye angali—Yeye angali analinda dhidi ya kuumwa na nyoka. Um-hum.

26 Mnaona, ndugu yake mwenye dhambi, mvulana mzuri, tunamshughulikia apate kuwa Mkristo. Sasa, mwenye dhambi alienda hospitalini, damu ile ile, mvulana yule yule, ndugu, akaenda hospitalini, akalazwa hospitalini, gango mguuni mwake, akatembea nalo muda mrefu. Naye huyu Mkristo, mwaminio huyo moja kwa moja alimkanyaga nyoka wa aina ile ile wala haikumsumbua hata kidogo. Mnaona? Naam bwana. Mungu akubariki, Ndugu Evans.

27 Ninamwona Ndugu na Dada Tom Simpson wameketi moja kwa moja nyuma yao. Moja kwa moja nyuma ya huyo ni Ndugu na Dada Fred Sothmann. Wao ni Wakanada, wamekuja hivi punde. Ndugu na Dada Collins. Mbona, hawa hapa Ndugu na Dada Dauch. Na hapa . . . Sasa, Ndugu na—na Dada Dauch wanatoka huko Ohio. Wamekuwa marafiki zangu kwa miaka mingi. Hawa hapa marafiki zetu kutoka hapa chini Tennessee, huendesha gari maili mia nne . . . mia nane kila ninapozungumza, wakija mkutanoni. Wote wanaohusiana na Maskani ya Branham, simameni tu kwa dakika moja, wanaohudhuria tu hiyo maskani. Hebu tuone ni wangapi bado wamewakilishwa. Texas, Louisiana, Georgia, na Carolina Kaskazini, New York, Ohio . . .

> Wanakuja kutoka Mashariki na Magharibi;
> Wanakuja kutoka nchi ya mbali. (Hiyo ni kweli?)

28 Hatimaye nilipata kukusikia, ndugu, ukiimba "Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu" jana. Hao jamaa kutoka huko chini Tennessee, Ndugu, ama, Dada Ungren, Dada Downing, yule ndugu, na ndugu, siwezi ka- . . . Myers, Dada Myers, na Joanne, na loo, loo, loo jamani, hao wote. Ninawapenda.

29 Nanyi mwajua, nilikuwa na ono muda si mrefu uliopita, majuma machache yaliyopita, kwamba nilikuwa nikihubiri kutoka kwenye jua, nami nilikuwa na kusanyiko kubwa. Nalo litatimia. Nami nilikuwa nikihubiri, na wasikilizaji wangu walikuwa ni ka—ka—kanisa kubwa msituni. Na jua nililokuwa nimesimama ndani yake lilikuwa likiangazia mahali pengi. Nilikuwa na vilele viwili vya kufikia, nami nilikuwa

nikiwaonyesha kuhusu uponyaji wa Kiungu, kuhusu maono, na jinsi ambavyo Mungu alikuwa ameahidi, na kila kitu. Nao walikuwa wakishangilia.

30 Lakini basi, nilipofikia kwenye upeo wangu wa kwanza, ilikuwa ni kuwaambia ya kwamba mambo haya yote yalikuwa ni Neno. Basi nilipofikia kusema hivyo, kila mtu akawa na njaa. Kweli mimi huhubiri kwa muda mrefu sana. Lakini walishikwa na njaa, walitaka kwenda kula chakula, nao wakaanza kuondoka.

31 Nikasema, "Ngoja kidogo. Hamjasikia. Mnaona, nataka kuwaambia linakotoka. Ni Neno, Neno." Basi nilipoanza kulisema, kuzungumza tena kuhusu Neno, na jinsi yalivyofanywa kwa Neno, kila mtu akaondoka. Naam, hivyo ndivyo ilivyotokea. Hmm. Niliposimama pale, Maandiko yakanijia, katika ono nikiwa nimeketi kwenye kiti, yapata saa tatu asubuhi moja nyumbani kwangu.

32 Halafu basi, mwajua, Bwana wetu, alipokuwa, huduma Yake changa, alipokuwa akiwaponya wagonjwa na kila kitu, Rabi huyo kijana kutoka Galilaya, Yeye alikuwa ni mtu mashuhuri. Lakini siku moja akaanza kushuka kwenye Neno. Naye alipoingia kwenye Neno, watu wakaondoka. Wale sabini wakamwacha. Ndipo basi akageuka, akawaambia wale thenashara, "Nanyi pia mtaondoka?" Hmm?

33 Ndipo basi ilitokea nikawazia katika ono langu, "Naam, hiyo ni kweli. Mnaona, ninacho kilele kingine, kilele kikubwa ambacho sina budi kukifikia. Mnaona? Lakini jua linawaka sana sasa. Lakini vivuli vya jioni vitakuwa vikianguka baada ya muda mfupi. Wote watarudi tena. Ndipo nitafikia kilele hiki kingine." Nikainua mkono wangu, nikasema, "Utukufu kwa Mungu. Haitanibidi kusoma tena, kwa maana agizo langu hapo mwanzo lilikuwa ni kudumu na Neno, nami nitadumu na hilo. Ndipo nitakapoanza tena, nitawekea msingi tu yale niliyosema, halafu basi ningojee kilele hiki." Nami nikawazia, "Sipaswi kusahau hilo." Ndipo nikatoka kwenye hilo ono. Sijui nilikuwa na so—somo gani. Lakini kuna kilele kingine kinachokuja, um-hum, hakika kabisa.

34 Nataka kuwaambieni nyote hapa. . .Sipati kuwaona kanisani sana, sababu kanisa letu ni dogo, na tumesongamana huko kama sijui nini, na mamia wakingojea, wakaja, wakarudishwa, na kadhalika, kutoka majimbo mbalimbali na kadhalika.

35 Lakini wakati Neno linapoanza kutolewa, ninataka kuwaambia awali (Mimi ni mchungaji mwenzi hapa, mnajua)— mbele ya kusanyiko hili, wakati Neno lilipoanza kutokea, mnajua Petro alisema nini? "Bwana, twende wapi?" Dumuni na Neno. Kulikuwa na wachache waliobaki.

36 Asanteni nyote kwa kushuka kuja. Sikujua hata mmoja wenu alikuwa anakuja, sikujua mmoja alikuwa anakuja, maana nilijua kungekuwa na msongamano mkubwa huku chini, nasi kwa namna fulani hatukuutangaza. Lakini tuna—tunashukuru mko hapa. Na hawa ni ndugu na dada zenu katika imani moja. Mnaona?

37 Hili ndilo kundi dogo la wasafiri kama ninyi mlivyo. Sisi ni wasafiri na wageni. Tunautazamia mji ambao Mbuni na Mjenzi wake ni Mungu, nasi ni wasafiri. Ninawapa mikono, na kujua jinsi wapishi hapa wanaweza kupika . . . kuoka biskuti vizuri. Na hakika mtapata uji wa shayiri. Nina hakika na hilo. Kwa hiyo tembeleaneni, na kupeana mikono, na mkafahamiane wakati mkiwa hapa. Sasa, Bwana na aongeze baraka Zake.

38 Ninataka kuwaambia jamaa wa maskanini hapa: hivi karibuni, sasa, hatujui, hawatataturuhusu kuliboresha kanisa hilo mpaka tuweze kununua maeneo ya kuweka vituo zaidi vya kuegesha magari. Wala hatuwezi kununua ardhi. Labda itatubidi kulihamisha. Huku kanisa likijaribu kunisaidia kulipia deni hili la dola elfu arobaini. Wataninii . . . Ilinibidi kukopa elfu tatu kutoka maskanini kuilipia hiyo, sehemu yake. Na kidogo ni vigumu kwetu kununua kanisa wakati huu.

39 Lakini niliahidi baada ya hizo Nyakati Saba za Kanisa tungezungumza juu ya ile Mihuri Saba ya mwisho. Mungu akipenda, tutafanya hivyo mara moja. Kwa hiyo tutawaambia kwa barua itakuwa lini, nanyi mpige simu na kumpata Billy, endapo mnataka kuwekewa chumba na kadhalika, ili awatafutie mahali pa kukaa. Mnampenda? Amina.

40 Ndugu Palmer, hivi majuzi usiku, yule ndugu . . . Jina lake ni nani, ninii . . . jamaa huyu mkubwa hapa, mume wa Judy? Ernie. Ernie. Jamani, nilifikiri Veck angeweza kuimba hilo *Amina*. Lakini hakika alikuwa na sauti kama ya nyukibambi katika jagi. Kweli angeweza tu . . . Mbona, sikumaanisha hilo hivyo, mwajua. Na—namaanisha, mnajua, kwa kilindi kabisa, kweli angeweza kuimba hilo. Jamani! Loo, hayupo hapa, sivyo? Ni sawa. Matamshi yangu fidhuli, hakuwa hapa kuyasikia. Kwa hiyo hiyo ni sawa.

41 Sasa, hebu tuanze sasa. Na kila mtu anayejisikia vizuri aseme, "Amina." Sasa, tutajaribu kuondoka adhuhuri kamili, Bwana akipenda, upesi tu tuwezavyo kuwa na wachache . . . ninii tu . . . Madarasa ya shule ya Jumapili yote yameruhusiwa kuondoka, sivyo, Ndugu Jack? Na ibada imekwisha, tutakuwa tu na ushirika mdogo pamoja sasa.

42 Na—nanyi mnajua ushirika ni nini? Ndugu Bosworth, ni wangapi wamewahi kusikia habari zake? Bila shaka nyote mmesikia. Aliniambia siku moja, akasema, "Ndugu Branham, unajua ushirika ni nini?"

Nikasema, "Mbona, Ndugu Bosworth, nafikiri najua." Nadhani ni mtakatifu mzee ambaye mlimfahamu.

43 Akasema, "Ni watu wawili katika meli moja." Hiyo ni kweli. Huo ndio ushirika, ushirika wa Baptisti uliotengwa. Mnaona? Tumeketi pamoja sasa katika mahali pa mbinguni katika Kristo Yesu, mahali pa mbinguni, tukishirikiana. . . katika Kristo kwa Neno Lake, tukishirikiana kwenye Neno. Hilo si linapendeza? Ushirika kwenye Neno, kila jambo kwa pamoja, tukiketi kwenye meza moja, tukipishana.

> Loo, Yesu ana meza iliyoandaliwa ambapo watakatifu wa Mungu wanalishwa,
> Anawaalika wateule Wake "Njoni mle;"
> Kwa mana Yake hutulisha na kutupatia mahitaji yetu yote;
> Lo, ni tamu kula pamoja na Yesu wakati wote! (Um-hum, hmm, hmm, hmm!)

Sasa, hebu na tuvifungue vikombe vye—vyetu na kupishana, ushirika na urafiki sisi kwa sisi, tunapolitazama Neno.

44 Katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, nimechagua, asubuhi ya leo, kifungu kidogo kinachojulikana kutoa muktadha kwake. Na sikuzote kanda hizi ziko sokoni, ama kwenye be—benchi. Wala sidhani wangeziuza Jumapili. Lakini ukitaka kuagiza moja, jambo fulani linaweza kusemwa, ungependa kuchunguza hiyo, ama, katika mstari wa maombi.

45 Sasa, jana usiku. . . Nataka kuomba msamaha kabla sijafanya hivi. Nilikuwa ninaenda kumsaidia Ndugu Moore kufanya ubatizo jana usiku, lakini nikaingia kwenye mstari huo wa utambuzi. Na, kwa kweli, sikumbuki kabisa kuondoka hapa. Sasa, hiyo ni kweli. Mnaona? Nimechoka. Nimepungua kutoka pauni mia moja na sabini hadi mia moja thelathini na tano. Kwa hivyo mimi ni. . . Lakini kwa kuwa mzigo umetoka mabegani mwangu sasa, labda naweza—naweza kwenda mbele vizuri zaidi.

46 Kama Ndugu Williams alivyosema hivi majuzi asubuhi kwenye kiamshakinywa cha Wafanya Biashara, alisema, Mayos walimwambia, wakasema, "Huna budi kuaga dunia, hivyo tu," miaka michache iliyopita. Na mara tu walipomwambia hivyo, aliikimbilia simu. Kasema, "Utaninii. . . unakufa tu. Una—unapoteza uzito." Ndipo akaikimbilia simu na kupiga. Naye Billy akamwambia ashuke aje. Wakamweka pale kwenye mstari wa dharura. Nikaingia ndani, nikazungumza naye kwa dakika chache, na kumwombea. Nadhani ameongeza takriban pauni sabini tangu wakati huo.

Kasema daktari alimwambia, kasema, "Sasa, unapaswa kupunguza baadhi ya uzito huo."

Akasema, "Kama Mungu ameniwekea huu, nitauacha ubaki hapa." Kwa hivyo nadhani hilo ni jambo zu—zuri.

Sasa, mnayo Maandiko yenu sasa, basi tunaweza kusoma? Yohana Mtakatifu m—mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, kuanzia kifungu cha 35:

> *Tena siku ya pili yake Yohana alikuwa amesimama pamoja na wawili katika wanafunzi Wake;*
>
> Akamtazama *Yesu akitembea,* akasema, *Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu!*
>
> *Wale wanafunzi wawili wakamsikia akinena, wakamfuata Yesu.*
>
> *Yesu aligeuka, akawaona wakimfuata, akawaambia, Mnatafuta nini? Wakamwambia, Rabi (maana yake, Mwalimu), unakaa wapi?* (Swali kweli kweli, sivyo? Unakaa wapi Wewe?)
>
> Naye *akawaambia, Njoni, nanyi mtaona.* Nao *wakaenda, wakaona akaapo, wakakaa kwake siku ile: kwa kuwa ilikuwa yapata saa kumi.*
>
> *Andrea, nduguye Simoni Petro, alikuwa mmoja wa wale wawili waliomsikia Yohana na kumfuata Yesu.*
>
> *Huyo* akamwona *kwanza Simoni, ndugu yake mwenywe,* akasema, *Tumemwona Masihi, maana yake, Kristo.*
>
> *Naye akamleta kwa Yesu. Naye Yesu akamtazama, akasema, Wewe ndiwe Simoni, mwana wa Yona: utaitwa Kefa,* maana yake, *Jiwe.*

47 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye usomaji. Mungu anakaa wapi? Makao Yake ni yapi? Tungejuaje kwamba tulikuwa nyumbani Kwake? Iko wapi? Na kama alivyowaambia wanafunzi hao, "Njoni, mwone." Hivyo ndivyo angetwambia asubuhi ya leo. Hawezi kubadilika. Hana budi kubaki yeye yule. "Njoni mwone." Sasa, nataka kutoa kwenye hili nipate kuzungumzia muhtasari kidogo nilioandika hapa, *Kushawishika Na Kisha Kuhusika,* nataka kufanya hilo kuwa ndilo somo.

48 Sasa siku hizi, tunaona, na kujua, na tunaweza kutazama wasikilizaji na wanaoenda, na ambalo tunashukuru kwa ajili ya marafiki zetu, na wapendwa wetu, na ndugu na dada wenzetu katika Kristo, lakini mbele ya hayo yote, lazima tukubali kwamba kuna mwanguko mkubwa.

49 Niliposimama pale asubuhi ya leo na kuongeza kipande kingine cha karatasi nyuma hapa, nilipomsikia huyu ndugu mwenye neema akizungumza, ni—niliongezea kitu kingine. Mnaona, ili kuthibitisha kuna kuanguka, hakuna angalau mlinganisho siku hizi na vile ilivyokuwa wakati huo. Mnaona, nnaona? Loo, hu—huenda tukawa na idadi kubwa zaidi. Tuna majengo bora zaidi. Jamani, hakika. Lakini kitu hicho *halisi*, kuna kuanguka kutoka kwacho. Hata hivyo, ha—hatutaki kuwazia hilo.

50 Lakini labda kama Mungu amewachukua baadhi yetu, kama vile tungesema, wanenaji, ama kitu fulani, ambacho tungeninii . . . Yeye hutuinua juu. Naye anatuli- . . . Alilinganisha katika agano Lake manabii Wa—Wake, Yeye aliwaita tai, Naye alijiita Mwenyewe tai. Yeye ni Yehova-tai. Nami naamini niliwahubiria hapa chini, mahubiri wakati mmoja juu ya *Tai Akitaharakisha Kiota Chake,* na hilo ndilo linalotakiwa kufanywa. Lakini Tai hana budi kufanya hivyo Mwenyewe. Mnaona?

51 Lakini mnaona, hakuna ndege anayeweza kumfuata tai. Loo, unasema, "mwewee." Mwewe huyo akijaribu kumfuata tai, angesambaratika angani. Um-hum. Asingeweza kumfuata huyo tai hata afanyeje (Mnaona?), maana huyo tai anaweza kwenda mbali sana hata mwewe hawezi kumfikia. Na kabla ya kwenda huko, hana budi kujengwa apate kustahimili.

52 Lakini kadiri unavyopanda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi, kama wanaanga, na kadhalika sasa. Mnaona? Kadiri unavyokwenda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi, ikiwa umetayarishwa kuona.

53 Sasa, ingemfaa nini tai kwenda kule juu, kama asingeweza kuona akiisha kufika kule? Kwa hivyo nafikiri hivyo ndivyo wengi wetu tunavyojaribu leo kujiinua katika kitu fulani, wakati hatujatayarishwa kwanza. Um-hum. "Ee Mungu, nipe karama ya *hiki*, na ufanye *hiki*, *kile*, *pale*." Huipati. Kwa nini? Hujatayarishwa kwa ajili yake. Hutafanya lolote jema baada ya kufika huko. Na wakati ukifanya hivyo, na ikiwa ulijaribu kujiinua juu, ungesababisha tu, kile ninachoita leo, kile ambacho kimelidhuru kanisa letu kuliko kitu kingine chochote, ulinganisho wa kimwili.

54 Jana usiku nilisimama kwenye vi—vipandio vya makazi yangu, maskini mwanamke mmoja amesimama pale akilia. Yapata miaka mitatu iliyopita katika mkutano wa Chicago, alikuwa ameketi pale, na alikuwa ndio kwanza afanyiwe upasuaji wa kutoa mji wa mimba, alikuwa ametolewa viungo vyake vyote, nayo kansa ilikuwa imeenea mwilini mwake. Daktari alikuwa amemkatia tamaa. Nao ni maskini Waarkanser wazuri huku juu, jirani zenu hapa juu, na kwa hiyo . . . Maskini mwanamke mzuri, na mumewe ni—ni Mpenteko- . . . , la, baba wa mumewe ni mhubiri wa Kipentekoste, naamini hivyo ndivyo ilivyokuwa, sasa, baba wa mumewe.

55 Basi, walikuwa wamesikia juu ya hiyo mikutano, nami nafikiri kupitia kwa Ndugu G. H. Brown ama chochote kile, nao walikuwa wamekuja Chicago na walikuwa wameingia na walikuwa wameketi huko nyuma katika hali ya kukata tamaa.

56 Roho Mtakatifu, kama mlivyomwona akifanya kazi jana usiku, alisogea moja kwa moja juu ya hilo kusanyiko kisha akarudi na kumwambia. Hilo hapo. Na ni wangapi waliowahi

kunisikia nikisema, “Ninaona uvuli mweusi juu yako, wa kufa”? Sasa, tunayo ile picha, kama tu vile tulivyo na ya Malaika wa Bwana, ya kitu hicho. Tunayo picha yake. Ilipigwa tu. Kazungumza na mwanamke aliyetiwa uvuli wa mauti. Wakaipiga picha. Basi walipoipiga, kwenye hiyo picha juu ya mwanamke huyo palikuwa na kifuniko cheusi cha moshi mweusi ukizungukazunguka. Mwepesi tu uwezavyo kuwa. Akiwa Southern Pines, North Carolina. Na hapo hiyo. . . Ninyi nyote, kanisa kutoka maskanini, mliiona kwenye ubao wa matangazo, sivyo? Naam. Vema. Hiyo hapo. Mnaona?

57 Sisemi uongo. Ni—ninaweza kusema uwongo, kwa sababu mimi ni mwanadamu. Lakini sidanganyi, kwa sababu Mungu anageuka moja kwa moja na kuthibitisha hilo kuwa ni kweli. Nilipowaambia kuwa kulikuwa na nuru, nikiwa mvulana tu huko chini mtoni wakati gazeti lilipoipiga pi—picha yake, na mnaona, sasa iko. . . Hilo limethibitishwa. Hilo limepita shaka lolote. Makanisa yote, watu wote, Wakristo, wanajua hilo. Mnaona, mnaona? Naam, ni u—uvuli. Ndiposa kifo kinapotokea, ni uvuli. Na hapo mwanamke huyo alitiwa uvuli wa mauti.

58 Vema, maskini mwanamke huyu pia alikuwa, naye Roho Mtakatifu akamwambia alikotoka. Ndipo nikatazama nyuma, na giza hilo lilikuwa limefifia, kulikuwa na Nuru ikining’inia juu yake. Ndivyo hivyo. Nami nitaweka tu maisha yangu pale pale kwamba ndivyo hivyo. Hajawahi kukosea. Kwa hiyo basi, neno likatoka, “BWANA ASEMA HIVI.” Sasa, mara nyingi ninyi nyote mnaopata maono hayo (Mnaona?), mnayapata kwa njia ile ile ambayo. . . Si ono, na hata hivyo, ni ono.

59 Mnaona, wakati yule mwanamke alipogusa upindo wa vazi Lake, huyo alikuwa ni mwanamke huyo akiitumia karama ya Mungu. Mnaona, alivuta kutoka Kwake, maana Yeye alisema, “Nimekuwa dhaifu.” Na kwa kweli hakusema, “Nilikuponya,” Alisema, “Imani yako ilikuokoa.” Neno *sozo*, kama vile tu, “wokovu wa kimwili, wokovu wa kiroho.” Mnaona? “Imani yako ilikuokoa.” Sasa, mnaona, huyo mwanamke, imani yake mwenyewe ilifanya hivyo, akiamini ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu.

60 Sasa, Mungu alipotaka kutumia karama Yake kwa Lazaro, Yeye alimpa tu ono. Akaondoka, na aliporudi akamfufua mtu kutoka kaburini ambaye alikuwa huko siku nne, tayari, kwa maneno yetu ya kujua jambo hilo, akioza. Pua yake ilikuwa tayari imebonyea, muda huo. Unaona? Vema. Sasa, na Yeye kamwe hakusema neno juu ya kudhoofika. Huyo alikuwa ni Mungu akitumia karama Yake.

61 Yule Mwingine alikuwa ni mwanamke akitumia karama ya Mungu. Basi hiyo—hiyo. . . Yesu hata hakujua alikuwa pale. Alikuwa akipita tu, Naye akageuka. Sasa, Yeye hakuwa mnafiki, mnajua, Yeye alisema, “Ni nani aliyenigusa Mimi?”

Hakujua. Ndipo akapata mahali ule mvuto wa imani ulikuwa, akamwambia "Imani yako imekuokoa: kutokwa kwako na damu." Mnaona? "Imani yako ilikuokoa."

62 Vema, hilo ndilo jambo lile lile linalofanyika hivi. Mara nyingi kama hilo likifanyika. . .sasa angalieni hilo. Lakini jukwaani, au mahali fulani ambapo nilimpata mtu kibinafsi ambaye ninaweza kuzungumza nao, na kuona wana shida gani, basi laiti tungeweza kungoja kwa dakika chache tu, na kuona kile Bwana anasema kuhusu jambo hilo!

63 Sasa, uwe na hakika ya kwamba huyo ni Mungu anayesema hivyo sasa, wala si dhana. Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, kuna hila nyingi sana katika Pentekoste. Um-hum. Hiyo ndiyo sababu u—u—u—u—unyofu na ujasiri umepotea, ni kwa sababu, uigaji wa kimwili. Kama tungekuwa na hakika huyo alikuwa ni Mungu, tungetulia tuli. Kwa hivyo tunaposema, "BWANA ASEMA HIVI," kuwa na hakika kwamba ni Mungu, si mawazo yako mwenyewe, au dhana, au mdundo. Jua kwamba ni Mungu. Na kisha katika kisa hiki lilimjibu na kumwambia. Mzima kabisa, amekuwa hivyo tangu wakati huo.

64 Siku chache zilizopita huko Arkansas kulikuwa na maskini mhudumu aliyekuja. Nami silipingi neno la mvulana huyo. Sina haki. Mimi si Mungu. A—alisema Bwana alimpa karama ya upambanuzi. Vema sasa, bila shaka, hiyo ni mojawapo ya karama za Maandiko, hakika. Hiyo ni sawa. Lakini unaona, aliyosema yalikuwa ni kinyume.

Alikuwa akimwambia, akishuhudia juu ya yale Bwa—Bwana alikuwa amemtendea.

65 Akasema, "Loo, lakini ngoja kidogo. Imekurudia tena." Vema, kama vile, ilimshtua maskini mwanamke huyo kabisa, naye huyu hapa jana usiku amesimama pale akilia. Tayari amebatizwa mara moja, naye huyu hapa kwenye orofa ya chini akijaribu. . .kuvaa joho, alikuwa ameshuka chini upesi kubatizwa ili afike nilipokuwa. Tayari amebatizwa, lakini alikuwa anaenda kubatizwa tena, kusudi tu, apate, asimame pale. Ndugu Jackson alikuwa barazani pamoja naye jana usiku nje hapa kwenye moteli yangu. Kwa kuwa yeye. . .Mvulana huyo akimwambia jambo hilo, naye mwanamke huyo hakuwa na kansa zaidi ya vile Jim Maguire alivyo nayo, anayeketi hapa. Unaona?

66 Mwanaume. . .Mmoja wa ndugu zetu wa Kipentekoste alikuwa kwenye mkutano ambapo ndugu mwingine mdogo alikuwa amekuja na kumwambia binti yake kwamba alikuwa akifa kwa kansa. Naam, akamleta kwa ndege. Nikaingia chumbani. Tukamweka pale katika hali ya dharura, na kumtazama Bwana. Nikamwona. . .Hii imekuwa kitambo kidogo, nami nikamwona akiwa amebeba watoto wawili. "Mbona," nikasema, "hufi. Huna kansa. Sasa, chukua tu. . .

Nitailipia, nenda kwa mtaalamu ukafanyiwe uchunguzi." Mnaona? "Huna kansa."

67 Kwa hivyo unaona, ni...Naye alinena katika Jina la Bwana. Mvulana huyu akafanya vivyo hivyo. Ni nini? Ni shauku, mhemuko. Na katika kufanya hivyo, hivi hamtambui ya kwamba—ya kwamba hilo linaweka kifuniko u—usoni mwa watu? hata hawajui la kuamini. Kuwa na hakika lile unalozungumzia.

68 Siku hii ya kuanguka, na kwa kuwa imeangukia hapo, watu wanapoteza kuhusika. Kumbukeni, huo mti unakua, vile vile tu. Kama Yoeli alivyosema, "Nitarudisha." Wengi wenu huchukua kanda, na laiti mngeupata ujumbe huo wa *Mti wa Bibi-arusi*. Mnaona? Hata hivyo ulikatwa. Na ule Mti mkuu, Kristo, ulikatwa. Yeye alikuwa ndiye ule Mti wa Uzima uliotoka katika bustani ya Edeni na ukatundikwa kwenye m—mti katili, mti uliotengenezwa na Warumi.

69 Lakini Mti ule ule wa Uzima aliokuwa, ambao mtu huula Huu na asife, Yeye alikuwa akimleta Bibi-arusi. Na wakati Bibi-arusi huyo alipotoka kwa Roho Mtakatifu, ni nini kilitukia? Ulikatiliwa mbali na Ukatoliki wa Kirumi katika dhehebu. Lakini Yoeli aliahidi ya kwamba ungerudishwa tena.

70 Ulianza tena kutoka kwenye kisiki katika siku za Luther. Alifanya nini? Akaliundia dhehebu. Ukakatwa tena, ukapogolewa. Huo Mti ukaendelea kukua. Ukaingia kwa Wesley. Nini ilifanyika? Kuundiwa dhehebu, kupogolewa, bwana wa hilo shamba la mizabibu akayapogoa hayo matawi. Yakafa. Nionyeshe wakati mmoja ambapo dhehebu lilipata kurudi tena. Yanapogolewa.

71 Ndipo ikaja Pentekoste, tawi lingine likitoka kwake. Ikawaje? Likaunda dhehebu, likapogolewa, likakatwa tena. Lakini kumbukeni, chini ndani ya moyo wa kisiki hicho, uta—utazaa Bibi-arusi halisi. "Nitarudisha," asema Mungu. Na huo mti, matunda yake, huivia wapi kwanza? Ni huko juu. Kwa nini? Ni karibu na jua. Afadhali niachane na hayo sasa. Tunarudi kwenye hili lingine.

72 Kuanguka, hakuna kuhusika. Ninaweza kuona wazo la watu, nami ninataka kuzungumza juu ya hili kwa sababu hii ni shule yetu ya Jumapili, na wakati ninii tu...kanisa letu moja lilipokutana hapa, makanisa mawili, makundi mawili lakini watu wale wale, kwa hivyo ni—ningeweza kueleza hili.

73 Kuna kuanguka, nako...na kule kuanguka kumesababisha kutohusika. Wanafanya nini siku hizi? Inaonekana kuwa, tangu Mtaa wa Azusa na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, kwamba jambo pekee ambalo ni muhimu kanisani ni kupata washiriki, washiriki zaidi, kuchukua chochote. Nasi tunatumia fundisho kwamba iliwabidi kunena kwa lugha ili wampate Roho Mtakatifu. Na ndugu wengi waliwashusha watu, wakawahimiza

warudie-rudie neno fulani, "utukufu, utukufu, utukufu," mpaka wakapata mkanganyiko wa lugha. Laiti wangelitulia tu mpaka Roho Mtakatifu aje!

74 Sasa, ninaamini mnanena kwa lugha pia. Ninaamini hilo. Lakini kama una Roho Mtakatifu halisi, wa kweli anayenena kwa lugha, unajua nini? Maisha ya Kristo yatafuatia ndani yako. Sasa, nimeona waganga wakinena kwa lugha. Nimeona mambo ya kila namna, nikiwa mmishenari, kunywa damu kutoka katika fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kunena kwa lugha, na kumwita ibilisi. Hmm.

75 Mama yangu mkongwe, ndio kwanza aage dunia miezi michache iliyopita, alikuwa Mhindi nusu. Nami nimekuwa katika kambi zao, na nimewaona wakijizungushia nyoka namna *hiyo*, na kucheza dansi ya mahindi, na kunena kwa lugha na kuweka penseli chini, nayo ingeandika katika lugha zisizojulikana na kuifasiri.

76 Kwa hiyo, unaona, hakuna mhemuko unaoweza kuweka juu ya Roho Mtakatifu. Ni kwa matunda yao mtawatambua. Sasa, hilo halikuondoi kunena kwa lugha, wala hilo haliondoi kupaza sauti, hilo huondoa. . .Maisha yako yanashuhudia, wewe mwenyewe. Yanakwambia ni—ni nini, maisha ya—yako yakilizungumzia.

77 Sasa, siku hizi jambo kuu ni kujiunga na kanisa, ushirika, ku—kusaidia kipindi cha redio. Vema, hiyo ni sawa. Mambo hayo, siyakosoi, lakini ninawaambia. Mnaona? Kujenga shule kubwa mahali fulani, hiyo si ni sawa? Kila mtu anataka kujenga shule ya theolojia. Wanataka pesa zote ambazo watu wanaweza kutoa kusaidia mambo kama hayo, na kuweka mamilioni ya dola ndani yake. Mnaona? Halafu basi, tabaka lili hili la watu linasema ya kwamba wanaamini ya kwamba Yesu anakuja katika kizazi hiki.

78 Je, hamjui? Watu si vipofu kabisa. Mbona, ushuhuda wako mwenyewe unashuhudia. Matendo yako yananena kwa sauti kubwa kuliko maneno yako. Unawezaje kusema kwamba unaamini Yesu anakuja, unataka kuweka jengo la dola milioni moja? Nao wamishenari, kweli, wasio na viatu miguuni mwao. Na kwa sababu wao si wa shirika fulani hawasaidiwi. Halafu tunasema kwamba tunaamini kuja kwa Bwana kumekaribia, "Atakuja katika kizazi hiki." Watu wanajua vizuri zaidi ya hapo. Mnaona?

79 Wana. . .hawajashawishika, hivyo tu, hawaliamini. Wanalichukulia tu kama desturi yao. Mtu fulani analisema, "Loo, Utukufu kwa Mungu. Yesu anakuja karibuni sana." Mwingine akasema, "Utukufu kwa Mungu. Yesu, anakuja hivi karibuni sana." Kama mnaamini hivyo, kungekuwa na kilio kikubwa sana humu jijini kuliko mlichowahi kusikia.

Ni desturi. Sio uhalisia kwa watu. Haininii—haininii . . . haifanikiwi. Inathibitisha haifanikiwi.

Hawajashawishika ya kwamba Yeye anakuja katika wakati huu, wala hawajashawishika tena kwamba Yeye yuko pamoja nao, hawajashawishika kabisa.

80 Sasa, Hawa hakushawishika kabisa kwamba Neno la Mungu lilikuwa kweli. Kama angeshawishika, hangeweza kamwe kusikiliza hoja ambayo Shetani alimpa. Ni vita viwili vikubwa. Vya kwanza vilipiganwa mbinguni. Shetani akatupwa nje. Naye Mungu ni mwanajeshi mkuu.

81 Sasa, mnaona, wakati taifa linapotuma wapelelezi kila mahali wapate kujua kile mtu huyo mwingine alicho nacho, vema, tunao wengi, ingawa tuna urafiki na Uingereza, kunao wapelelezi wa Uingereza hapa kuona siri zetu za atomiki, na kuna wapelelezi wa Marekani kule Uingereza wanaoona walicho nacho pia. Hakuna kuaminiana, kwa sababu mtu akipata kitu kimoja, huyo mwingine anajaribu kutafuta kitu kingine cha kukabiliana na hicho. Ndivyo wanavyoishi.

82 Mungu, kwa jeshi Lake, ambalo anajua . . . Na kila taifa linajaribu kuliandaa jeshi lao kwa yaliyo bora zaidi. Lazima wafanye hivyo wapate kuendelea kuishi. Naye Mungu akiliandaa jeshi Lake, akiwa hana kikomo, alijua silaha bora zaidi zilizokuwako. Naye alifanya nini? Aliwapa jeshi Lake Neno Lake. Hatujalindwa nyuma ya dhehebu. Hatujalindwa nyuma ya vikundi. Tumelindwa na Neno la Mungu. Naye ibilisi alijua hilo, kwa hiyo alijaribu katika ninii pekee . . . na sasa . . . Yule mpelelezi, ibilisi akijaribu kutafuta njia ya kuingia kwenye ukuta huo, huenda alijaribu anasa, huenda alijaribu kila kitu, lakini unajua alimpata Hawa wapi? Juu ya hoja.

83 Biblia ilisema tunapaswa kutupilia mbali hoja. Imani hufanya hivyo. Sasa, hoja. "Je, si ni jambo la busara, Ndugu Branham, ya kwamba kanisa liko katika hali nzuri zaidi leo kuliko lilivyokuwa kwenye Mtaa wa Azusa, ama huko nyuma katika wakati huo?" La, bwana. Wameliacha Neno. Wameacha . . . mahali ngao—ya—ya—yao. Neno ndilo Kinga yetu. Na ingawa watu hawangethubutu kusema hawakuliamini, wanalidai, lakini vitendo vyao vinanena kwa sauti kubwa kuliko maneno yao: mtu anaposema, "Loo, utukufu kwa Mungu, tunamtazamia Yesu aje wakati wowote; kusema, ni—nilininii . . . tutajenga jengo hapa nje, lina thamani ya dola milioni *kadhaa*."

84 Sasa, mnajua mbili mara mbili ni nne. Mwanafunzi yeyote wa darasa la pili angelijua hilo. Mnaona? Na unawezaje kuamini kwamba Yeye anakuja sasa kisha ujenge majengo makubwa?

85 Na hata hivyo, tunaona Uwepo wenyewe wa Kristo katika kutimizwa kwenyewe kwa Neno Lake. Lakini hatujashawishika kwamba ni Yeye (Hiyo ni kweli.), maana ulinganisho wa kimwili na kadhalika umewaacha watu bila tahadhari. Imefikia ambapo

karibu hakuna heshima, kwa jumbe. Na chochote tu kitainuka wanakiita ujumbe, wakati ujumbe unapaswa kuandikwa chini. Na kama hautimii, mna pepo mchafu hapo.

86 Mungu alisema, "Akiwepo mmoja miongoni mwenu ambaye ni wa kiroho au nabii, Mimi, Bwana, nitasema naye. Na kama hayatatimia basi si Mimi. Um-hum. Lakini yakitimia, basi mwogopeni, kwa maana niko pamoja naye," maana Mungu ni kweli.

87 Tunainuka tu. Nawe utaona, imekuwa ninii tu. . .kama matope. Hiyo ni kweli. Sasa, hilo ni neno baya sana kusema, lakini hii ni shule ya Jumapili. Hebu tulinyoshe hili. Ni yubile. Ni. . .mnaona, imefikia tu mahali hapo. Nimelitazama. Nimeliangalia papa hapa maskanini. Ninaliangalia katika maskani yangu. Ninaliangalia kila mahali.

88 Bila shaka, kama ono lilivyosema, wao wanaliacha tu. Haina budi kuwa hivyo. Kama walimfanyia Yeye, wakafanya hivyo vingine, watalifanya tena (Mnaona?), kwa sababu wanachukua hoja: "Sasa, hivi hatupaswi kuwa na *hii*?" Na, "Je, hatupaswi kuwa na *ile*?" Hizo ni hoja wala si Neno.

Sasa, unasema, "Naam, unajuaje?"

89 Vema, lipeleke tu kwenye Biblia, uone kama Mungu analithibitisha au la. Kama Mungu alitoa ahadi, Mungu hana budi kuitimiza ahadi Yake. Asipoitimiza, Yeye si Mungu. Sasa, huwezi kamwe kubahatisha hilo. Huna budi kumwamini Yeye kabisa, na afadhali ujue unachozungumzia. Sasa, wanalidai, lakini matendo yao yananena kwa sauti kubwa kuliko neno.

Mnajua, Yesu alisema, "Kama unanipenda, lisha kondoo Wangu."

Sasa, kamwe Yeye hakusema, "Wakate manyoya."

"Walishe."

Kamwe hakusema, "Waelimishe."

Alisema, "Walishe."

90 Vema, kondoo hulishwa ipasavyo kwa chakula cha kondoo; nacho chakula cha kondoo ni Neno. "Kwa maana mwanadamu hataishi kwa neno pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Sio moja tu hapa, mara kwa mara, bali kila Neno, "mstari juu ya mstari, hapa kidogo na pale kidogo," kila Neno Lake. Wape Chakula cha kondoo.

91 Nacho Chakula wanachotafuta ni Uzima. Kondoo halisi hutafuta Uzima. Na kuna Kitu kimoja tu kilicho na Uzima. Yesu alisema, "Maneno Yangu ni Uzima." Yeye ni Neno, na Yeye ni Uzima. "Mimi ndimi Njia, Mimi ndimi Kweli, Mimi ndimi Uzima." Naye ni Neno. Um-hum.

92 Sasa, tutawapaje kanuni ya imani? Mbona, unawapa magugu, magugu ya kimadhehebu, kanuni za imani, badala ya

Chakula cha kondoo, Neno. Nawe unakuza nini? Vema, kile tu magugu huzaa, bila shaka.

93 Yohana Mbatizaji wakati . . . Tuna taarifa ndogo ya Yohana. Jambo pekee tunalojua ni kwamba alikuwa mwana wa kuhani, na baba na mama yake walikuwa wakongwe. Na alipokuwapo, Zakaria, alikuwa akifanya kazi yake hekaluni, kama vile kutikisa chetezo wakati watu walipokuwa wakiomba, tunajua kwamba Malaika wa Bwana alimtokea na kumwambia kitakachotokea. Halafu basi, walikuwa wakongwe. Lazima iliihuzunisha mioyo ya huyo mume na mke wakongwe walipojua kwamba Yohana, yeye . . . kwa kawaida hawangeishi wapate kumwona akiingia katika uwezo wake. Lakini walijua ya kwamba angekuwa mtumishi mashuhuri wa Kristo, nabii.

94 Sasa, ni ajabu, sasa. Ikiwa baba huyo, akiketi chini na kumwambia Yohana, “Yohana, mwanangu, ulipozaliwa, jambo la ajabu lilitokea.” Mnaona? Jambo la ajabu lilitokea: Yohana akiwa amezaliwa kwa ajili ya kazi hiyo, badala ya kushuka kwenda shuleni ambako baba yake alitoka, ambayo ilikuwa ndiyo desturi kabisa, mvulana anapaswa kufuata mkondo wa baba yake. Hata, yeyote kati yenu anajua, katika kusoma kwe—kwenye, kwenye kanisa la Nikea, kama vile Mtakatifu Martin, baba yake alikuwa mwa—mwanajeshi. Yeye kabisa, ilibidi afuate mwelekeo wa baba yake—mwelekeo wa baba yake na kuwa mwanajeshi.

95 Na ilikuwa ni desturi ya siku hizo, kwamba walifuata aliyofanya baba yao. Hivyo ndivyo kuhani kutoka katika ukuhani wa Walawi, Lawi, mmoja alimfuata mwingine, ni ukoo wa ukuhani. Na wengine walikuwa wafuga kondoo, na wengine wafuga ng’ombe, na kila mtu alifuata mwelekeo wake, lakini Yohana, ajabu, badala yake, akijua kwamba kazi yake ilikuwa muhimu . . .

96 Sasa, hapana shaka kama angeenda shuleni mwao ambamo babake alitoka, “Naam, huyu ni—huyu ni mwana wa Zakaria. Kwa hivyo ninawaambia tutakalofanya. Tutaninii . . . Nawaambia tutakalofanya. Tutamfanya mtu mkuu miongoni mwetu namna hii, kwa sababu baba yake alikuwa mtu mashuhuri. Tutampa elimu yake, na Ph.D. yake, na yote namna hii.”

97 Yohana alijua kama angeingiziwa hayo ndani yake, angepoteza thamani halisi ya wito wake. Kwa hiyo yuaenda nyikani na kungoja, kwa sababu alijua ya kwamba angemtambulisha Masihi. Alijua basi jambo lile lile tunalopaswa kujua siku hizi, kwamba kuja kwa Masihi kulikuwa kumekaribia, kama tunavyoamini siku hizi.

98 Yohana kamwe hakuanzisha shule zozote, bali alihusika kuhusu Neno la Bwana. Naye angeweza . . . Baada ya kuhusika, alijua ilimbidi kushawishika mahali ambapo Masihi huyo

angekuwa. Naye alishawishika sana alipotokea, akasema, "Kuna Mtu aliyesimama kati yenu ambaye hamumjui." Loo, ndugu. "Mtu, sasa hivi, amesimama kati yenu. Hamumjui, lakini Yeye Ndiye. Nitamjua, kwa sababu nimeshawishika kwamba siwezi kukosea. Mungu aliniambia huko nyikani ningemjua, kwa maana ningeona ishara juu Yake, ishara ya Kimasihi."

99 Mmoja wao huenda alimjia, mmoja wa hao makuhani wakuu, na kusema, "Bwana, tunakuchukulia kuwa nabii. Huyu hapa Ndugu Fulani-wa-fulani. Yeye ni mtu mzuri sana. Mbona, yeye ni mmoja wa marafiki wakubwa sana wa kuhani mkuu. Ni jamaa mzuri sana. Hivi hufikirii, bwana, hivi hufikirii, sasa, kuwa mwaminifu, je, hufikirii kwamba yeye ndiye Masihi?"

"La."

"Vema, hufikirii kwamba tunapaswa kumfanya . . . "

100 "Sijui lolote kuhusu hilo." Lakini akasema, "Nitamjua, kwa maana Yeye aliyeniambia nyikani niende nikabatize kwa maji, alisema, 'Ambaye nitamwona Roho akishuka juu Yake, huyo atakuwa Ndiye.'"

101 Sasa, hakusema, "Sasa, nitakwambia tutakachofanya. Tutaanzisha shule. Tutaelimisha kundi la watu katika hili." La, bwana. Muda ulikuwa umeenda sana. Hakukuwako na la kufanya ila kujiandaa. Lihubiri Neno; iangalie ishara.

102 Ndipo basi alipotoka kule siku moja, naye alikuwa amesimama ng'ambo ya mto akihubiri, naye kuhani mmoja ng'ambo ya pili akasema, "Naam, Rabi, unataka kuniambia kuna wakati ambapo dhabihu ya kila siku itakoma katika hekalu, nao hawatakuwa na wana-kondoo tena?"

Akasema, "Utakuja wakati ambapo mtu mmoja atakuwa Mwana-Kondoo wa Mungu."

"Loo," wakasema, "Rabi, umerukwa na akili."

Akasema, "Hapo . . . Loo, tazama, Huyo hapo. Huyo Ndiye."

"Una uhakika jinsi gani? Umeshawishika jinsi gani?"

103 Kwanza, alihusika juu ya . . . jinsi angejua. Na ndipo alipopata kujua hasa ingekuwaje, basi akashawishika ya kwamba huyo alikuwa Ndiye. Aliliona. Kwa nini hatuwezi kuliona leo? Wakati Mungu alipotabiri mambo haya kuja, hata kanisa la Laodikia, na utendaji wa Roho katika siku hii, tunapaswa kuhusika juu ya mambo haya, na ndipo tutashawishika. Kusingeweza kuwa na kosa.

104 Tunaona sasa kwamba mwanafunzi huyu . . . Baada ya Yohana kutoa tamshi hili, na kumwita atoke papa hapa, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu," Andrea alikuwa amesimama pamoja nao. Naye Andrea akamfuata Yesu kwa sababu alimwamini Yohana, akiona unyofu wake, ya kwamba atamtangaza Masihi.

Ndipo alipofanya hivyo, akasema, "Rabi, unaishi wapi?"

105 Naye Yesu akasema, "Njoni, mwone. Njoni, mwone ninakoishi." Naye akakaa Naye usiku huo. Alikaa Naye mpaka aliposhawishika ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi.

106 Shida yake ni kwamba, hatukai muda mrefu kutosha. Hatujashawishika. Hiyo ndiyo sababu kuhusika kwetu kumetuacha. Hiyo ndiyo sababu tunashughulika sana na mambo ya ulimwengu. Hiyo ndiyo sababu hatuna utulivu. Bado hatujashawishika kabisa. Tunadhani tumeshawishika. Lakini unaposhawishika kabisa, kama maskini yule ndugu alivyosema muda mfupi uliopita, jambo fulani linatukia. Unaposhawishika kweli, basi unahusika.

107 Sasa, mnakumbuka, Andrea, mara tu alipogundu-... shawishika, alihusika juu ya kaka yake. Alitaka kaka yake ajue kitu kuhusu hilo. Huwezi kutulia nalo. Huna budi kufanya kitu juu yake. Stefano alishawishika. Sasa, tunaona, unaposhawishika basi unahusika. Na hiyo ndiyo sababu nimeshawishika sana ya kwamba kanisa liko katika eneo hili la Laodikia, na hiyo ndiyo sababu ninahusika kulihusu.

108 Si kwamba siyapendi mambo haya, ni kwa sababu kwamba nimeshawishika kabisa kwamba ninasema ukweli kutoka kwa Neno la Mungu. Ninatazama mienendo Yake. Ninajiona nikifanya mambo, nashangaa ni kwa nini, ndipo ninaangalia nyuma na hili hapa. Anazungumza nami, nami ninashangaa, "Sikuwahi kuwazia hilo. Kwa nini hapa, hilo ndilo hasa." Ndipo ninashawishika, na hiyo ndiyo sababu ninahusika.

109 Sitaki mtu yeyote apotee. Ninahusika kukuhusu wewe. Ninahusika kuwahusu watu, kwa sababu nimeshawishika kwamba Yesu ndiye Kristo. Nimeshawishika kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Hiyo ndiyo sababu mimi, vema, huko uwanjani, nilianza miaka mingi iliyopita. Ningeweza kuwa milionea maradufu. Ati mimi nikope dola elfu arobaini? Hiyo ingekuwa "pesa kidogo," kama tusemavyo.

110 Kwa nini? "Kwa nini hukuzichukua?" Mchungaji wenu hapa anajua kwamba ni elfu ngapi mara maelfu mara maelfu ya dola tulizokataa. Kwa nini? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Nimeshawishika kwamba tuko mwisho, nami ninahusika juu ya hali ya kanisa hapa mwisho.

111 Nimeshawishika kuhusu wanawake kukata nywele zao. Ninahusika juu yake. Wao ni dada zangu. Nimeshawishika juu ya wanaume kuwa vibaraka. Ninahusika kuhusu ndugu zangu. Si kwamba siwapendi; kweli nawapenda. Hiyo ndiyo alama hasa kwamba nawapenda, sio kwamba ninajaribu kuwagombeza. Nimeshawishika, na ninahusika juu yake.

112 Sasa, sote tunapaswa kushawishika. Na tuliposhawishika, maisha yetu yanaanza kuwaka moto, kama vile yule ndugu alivyosema. Kuna kitu, hatuwezi kusimama kimya kukihusu.

Huna raha. Wewe tu, kama alivyosema muda mfupi uliopita, asingeweza kulala usiku kucha. Alishawishika kwamba huyo alikuwa ni Mungu. Alihusika juu ya kumpata yeye mwenyewe. Mnaona ninaloomaanisha? Kushawishika, kisha kuhusika.

113 Naam, Yohana alikaa nyikani mpaka alipopata kujua mpango wa Mungu ulikuwa nini. Ndipo akahusika. Alijua ishara yake. Andrea alikaa usiku kucha pamoja na Yesu, na ndipo akahusika kuhusu ndugu yake. Alienda akamleta. Ni mara ngapi tunaweza kutaja haya, ambayo, kabisa hatuna wakati mwingi zaidi huko juu, lakini na—nataka kusema maneno haya machache zaidi, kama mtanivumilia kama dakika zingine kumi.

114 Yakobo alikuwa na mdundo wa moyo kwamba hana budi kurudi nyumbani, bali alijua ilimbidi kukabiliana na adui wake. Hakujua jinsi atakavyofanya hivyo. Alifanya nini? Kwanza, alikaa hapo mpaka akamshika Mungu. Ndipo aliposhawishika kwamba alikuwa amepata baraka kwa sababu Mungu alisema hivyo, basi akahusika.

115 Kwanza lazima akae mpaka atakapojua jambo fulani limetukia. Alikuwa na alama katika utu wake wa kimwili ambayo ilionyesha kwamba Mungu alikuwa ameiweka juu yake. Huyo mkubwa mno, mwenye nguvu, vema, alikuwa—alikuwa Yakobo upande huu wa mto, mwoga mkubwa mno, mwenye nguvu, mwenye afya nzuri; na ng'ambo ya mto alikuwa Israeli anayechechemaa. Ng'ambo hii ya mto alikuwa mtu mwenye nguvu, Yakobo, mdanganyifu. Na ng'ambo ya pili ya mto alikuwa shujaa anayechechemaa, asiyeogopa chochote. Hata hakutaka kitu chochote ambacho Esau angeweza kumpa. Alishawishika kwamba alikuwa ameguswa na Mungu. Kila hatua ilimfanya tofauti.

116 Wakati mtu ni, kwa udhahiri sana anaona tofauti ya alama ya Roho Mtakatifu katika maisha yake, basi umeshawishika, nawe unahusika. Unapomwona mtu anayefuata, Yakobo mkubwa mwoga amesimama *hivi*, "Vema, Mungu abarikiwe. Mimi ni Dk. *Nanii* kutoka *ninii*," Loo, ndugu, shuka na uchechemee kidogo. Bila shaka.

117 Shamgari, wengi wenu . . . Alikuwa mmoja wa waamuzi wa Israeli, maskini nanii . . . Wahudumu wengi hata hawaoni hilo katika Biblia, lakini alikuwa mmoja wa waamuzi wa Israeli, mstari mmoja mdogo uliandika juu yake. Lakini ninampenda. Alikuwa mtu anayeupendeza moyo wangu.

118 Mwajua, Wafilisti, basi, kila mtu alifanya alichotaka kufanya. Kwa hiyo tunaona ya kwamba Waisraeli walikuwa wamekuza mazao mengi sana, nao Wafilisti wangekaa kitako kule nyuma, na kucheza kamari, na kuwaacha wawatumikie. Nao hapa wangeingia moja kwa moja, (hakuna umoja kati yao), wanaingia moja kwa moja na kusema, "Vema . . ." wanachukua mazao yao. Mwaka baada ya mwaka walifanya hivyo.

119 Maskini jamaa huyu mzee, siku moja, hakuwa a—askari wa vita, alikuwa tu na . . . kitu pekee alichokuwa nacho ni mazao yake. Nami ninamwazia akisimama baada ya kuweka mazao yake ghalani, akaangalia, watoto wake wenye matambara, naye mkewe alihitaji mavazi. Basi akayaweka yote humo ndani vizuri. Alikuwa amesimama pale, akiinama, akisema, "Vema, labda tunaweza kula msimu huu wa baridi kali."

120 Akasikia kitu fulani. Akachungulia nje ya dirisha la ghala, hawa hapa Wafilisti elfu moja wanakuja, taratibu, taratibu, taratibu, mabamba makubwa ya silaha juu yao, watu wakubwa, waliofunzwa vizuri, mikuki mikononi mwao, wakija taratibu kuchukua alichokuwa nacho.

121 Akaangalia chini, watoto wake. Akamtazama mkewe. Akahusika. Lakini jambo ni kwamba, alikuwa hajiwezi. Yeye si hodari wa kupigana kwa upanga. Sasa, hakusema, "Aisee, ngoja kidogo. Labda afadhali niende shuleni na kujifunza jinsi ya kupigana kwa kanuni za imani." Kama angefanya hivyo, hayo ndiyo tu angejua kuyahusu. Lakini hili hapa jambo moja alilojua: ikawa aliwazia, "Kwa kuzaliwa mimi ni Mwisraeli, na Mungu alimwahidi Ibrahimu baba yangu, kwamba uzao wake utamiliki lango la adui wake." Amina. Hilo latosha. Amina.

122 Alihusika kuhusu familia yake; alishawishika kwamba alikuwa Mwisraeli. Kitu cha kwanza alichokuwa nacho mkononi mwake, alikinyakua. Lilikuwa konzo la ng'ombe, fimbo, kipande kidogo cha shaba nchani mwake; la kutoa tope kwenye jembe, kulisukuma hilo konzo, au, ninii . . . kumchokoa ng'ombe wakati akitembea.

123 Nao Wafilisti elfu moja wenye silaha, haoni huo upinzani. Alihusika, ndipo akashawishika. Alishawishika, na alijua ya kwamba yeye alikuwa Mwisraeli. Alishawishika kwamba Mungu hawezi kusema uongo. Alishawishika kwamba hizo baraka zilikuwa juu yake. Alijua kwamba ilikuwa ni ahadi ya Mungu. Amina, ndugu. Ningeweza kujisikia kubarikiwa sana sasa hivi. Alishawishika kwamba ilikuwa ni ahadi ya Mungu, kama tu vile Matendo 2:38 ilivyo ahadi ya Mungu.

124 Alishawishika kwamba Mungu alisema uzao wake, ambao alikuwa, utamiliki lango la adui. Kwa hiyo akalinyakua hilo konzo la ng'ombe, akasimama pale pale nje, na kumpiga akambwaga chini kila mmoja wao. Kwa nini? Alihusika, naye alishawishika. Kweli. Kamwe hakungoja, sasa, kujifunza kanuni zote za imani, na kila kitu, na jinsi ya kupigana, na "Lazima niwe askari wa vita."

125 Hiyo ndiyo shida siku hizi. Hawashawishiki wakisha kujifunza. Sisi—sisi . . . Kijana mwanamume siku hizi anataka kwenda shuleni. Na Wapentekoste wetu, wanafanya nini? Jambo la kwanza, inawabidi kumpeleka shuleni karibu miaka kumi kupata Shahada yake ya Sanaa (Hiyo ni kweli.), seminari fulani.

Naye anapotoka huko, inambidi kujifunza taratibu zote za dini, ndipo anapotoka, bado hajashawishika.

126 Unajua, Mungu aliwatayarisha watu, walioshawishika vizuri zaidi, katika siku kumi kuliko tunavyoweza kuwafanya katika miaka kumi. Wakati seminari zetu, wanapotoka, bado hawajashawishika, kwa sababu walishindiliwa mapokeo. Lakini walipomngoja Mungu siku kumi, bila shaka walishawishika wakati huo. Bila shaka walishawishika. Baadhi yao kwenye Pentekoste wasingeweza hata kuandika majina yao wenyewe. Lakini walishawishika kwamba ilikuwa ni Mungu. Walijua ilikuwa. Wange—wangelifia jambo hilo. Walijua kwamba ilikuwa ni Mungu. Walishawishika. Naam.

127 Kwa hiyo walishawishika kuhusu Ujumbe Wake. Walishawishika kuhusu kazi Yake. Na jambo lingine, walishawishika: Haikuwalazimu kutoka nje, na wengine wanasema, "Sasa, ngoja kidogo. Ulitoka shule gani ya elimu? Sasa, ngoja kidogo. Utaendaje bila kadi ya ushirika? Utafanya nini?" Walishawishika. Nitasema jambo fulani: Walishawishika kwamba Yeye ndiye yote waliyohitaji.

128 Hatujafika mahali hapo bado. Um-hum. Naam. Walishawishika. Hawakuhitaji elimu. Walishawishika kwamba hawahitaji kadi yoyote ya ushirika. Walijua—walijua walikuwa ni uzao wa Ibrahimu, ya kwamba Mungu anaweza kutimiza yale aliyoahidi kufanya. Yeye alishawishika kwamba Yeye ndiye yote waliyohitaji. Hawakutaka dawa yao ya kimadhehebu ya kufanya mwili usioze. Tayari walikuwa wamedungwa sindano. Hum, um-hum. Nao walishawishika kwamba ilitosha kuwatunza. Walishawishika kwamba hiyo tu ndiyo waliyohitaji.

129 Na hili hapa jambo lingine, kama maskini yule ndugu alivyoniambia jana. . . Nilimwambia, nikasema, "Labda sarufi yangu ni mbovu."

Kasema, "Naam, nakwambia. Watu hawatambui. Sidhani kama wanaizingatia sana." Huh.

130 Hao ndugu waliotoka kwenye Pentekoste kule juu, walishawishika ya kwamba Yeye alikuwa ndiye yote waliyohitaji, nao walishawishika ya kwamba hilo tu ndilo watu walilohitaji, ilikuwa ni Yeye. Nami nimeshawishika jambo lile lile. Sijashawishika. . . Hawaniambii tu kwamba inanipasa kuzungumza vizuri zaidi, na inanibidi kufanya *hivi*, na kufanya *vile*, na kuwa na ninii bora. . . kusimama kimya nyuma ya mimbara kutoa. . . Hiyo ni saikolojia.

131 Unasema, "Naam, tabaka bora la watu huhudhuria." Tabaka la Mungu litahudhuria. Anafanya kazi pande zote mbili za mstari. Nimeshawishika kwamba watu hawahitaji mlolongo mkubwa, mrefu wa *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Nimeshawishika, kwa sababu ninajua kile lilichonifanyia, nimeshawishika litawafanyia vile vile. Naam, bwana. Nimeshawishika kwamba

atatimiza mahitaji yao yote. Nimeshawishika kwamba atatimiza mahitaji ya wengine wote.

132 Nilikuwa nikisoma hapa si muda mrefu uliopita kuhusu Hudson Taylor. Wengi wenu mmesoma habari zake, yule mmishenari mkuu nchini China. Kulikuwa na kijana mwanamume aliyemjia siku moja, yapata . . . mvulana, mwenye umri wa takriban miaka kumi na minne, kumi na mitano. Akasema, "Bw. Taylor, ninaamini nina wito maishani mwangu kuwa mhudumu. Nitakapofikia yapata umri wa miaka ishirini na mitano," akasema, "unajua nini? Ninakuja, nijiunge na shule yako, nami ninataka kujifunza."

Bw. Taylor, yule mwungwana Mkristo, akasema, "Mwanangu, usingoje hata huo mshumaa umeungua nusu. Nenda wakati umewashwa."

Hiyo ni kweli. Huhitaji masomo yoyote ya *hili* na masomo ya *lile*.

Unasema, "Vema, mshumaa umewashwa hivi punde tu."

Naam, wakati unapowashwa.

"Naam, sijui theolojia yoyote."

Huna haja ya kujua. Nenda uwaambie jinsi ulivyowashwa. Labda itawatia moto.

133 Tunachohitaji ni wakati wa kuuwasha mshumaa, nguvu za Roho Mtakatifu, badala ya mafundisho haya mengi ya sharti yaliyobuniwa na mwanadamu, mafunzo ya kitheolojia. Nami nimeshawishika hilo ndilo watu wanalohitaji. Kama yeye . . . anajua ABC zake au la, kama anajua kutofautisha maharagwe na kahawa iliyopasuliwa, ikiwa ataacha tu mshumaa huo uwashwe, Mungu atashughulikia hayo mengine yote. Hiyo ni kweli. Nimeshawishika kwamba hayo ndiyo yote anayohitaji.

134 Yule kipofu ambaye Yesu alimponya, asingeweza kubishania theolojia ya makuhani. Walikuja, makuhani wote wakakaribia, wakasema, "Unajua, huyu hapa Dk. *Nanii*. Wewe ni mfuasi wa kanisa fulani." Asingeweza kubishania theolojia yao. Wakasema, "Vema, tunajua mtu huyu ni mwenye dhambi. Tunajua ndivyo alivyo. Hakubaliani na mafundisho yetu. Anafanya nini? Anawahadaa watu wetu. Anawapoteza. Tunajua yeye ni mwenye dhambi." Ndugu, asingeweza kuibishania theolojia, lakini alikuwa na hakika kwamba angeweza kuona. Hiyo ni kweli.

135 Nafikiri hilo ndilo jambo kuu leo. Siwezi kukwambia mahali ninapopaswa kuwa, na ambapo sisi . . . huna budi kuwa *hivi*, ama kuwa *vile*; lakini bila shaka tumeshawishika kwamba tuna kitu fulani. Kama maskini yule bi-kizee mweusi alivyosema, kasema—kasema, "Ndugu, na—nataka kutoa ushuhuda."

"Naam, endelea, dada."

136 Akasema, “Mnajua nini?” Kasema, “Si—si—siiko vile ninavyopaswa kuwa,” akasema, “wala—wala—wala—wala siiko vile ninavyotaka kuwa.” Lakini akasema, “Jambo moja ninalojua hakika, siiko jinsi nilivyokuwa.”

137 Kwa hivyo nafikiri hiyo ni nzuri. Si—siko vile ninavyotaka kuwa. Siko vile ninavyopaswa kuwa. Lakini najua mimi siko nilivyokuwa, pia. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Angalau mshumaa umewashwa. Amina.

138 Daudi, mbona, yeye alikuwa ndiye mdogo kuliko wote je—jeshini siku hiyo, jamaa mdogo mwekundu. Alikuwa ndiye asiyefunzwa kuliko wote. Lakini alikuwa ameshawishika ya kwamba Mungu ambaye alimtumikia, kwamba alikuwa amepata tukio, kwamba angeweza kumwua simba aliyemshambulia, angeweza kumwua dubu aliyekuwa akijaribu kumwua. Naye alishawishika kwamba Mfilisti huyo asiyetahiriwa alikuwa akimfanyia uharibifu mkubwa Mungu wake na jeshi lake, “Yeye anaweza kumtia mikononi mwangu.” Amina. Loo, jamani!

Sauli akasema, “Ngoja kidogo, mwanangu. Nitakupa mafunzo kidogo. Nitakupa Shahada ya Sanaa katika dakika chache. Jaribu kuvaa ngao yangu.”

139 Ilimlemea tu huyo jamaa mdogo. Akasema, “Nivueni kitu hiki.” Aligundua kuwa fulana yake ya kikanisa haikugonga ninii. . . haikumwenea mtu wa Mungu. Akasema, “Acheni niende vile nilivyoenda hapo awali.” Hiyo ni kweli.

140 Loo, kama kanisa hili leo litaenda katika Louisiana jinsi lilivyoanza kwenda miaka hamsini iliyopita, mtamwua kila ibilisi anayekuja mbele zenu. Ni ahadi ya Mungu. Hamna budi, kushawishika kwamba Kristo yu pamoja nanyi nyote. Huna budi kushawishika, ndipo unahusika kuhusu wengine.

141 Samsoni alikutwa kwenye. . . nje kondeni na Wafilisti elfu moja. Akaangalia. Hakuwa na kitu mkononi mwake. Maskini mduvi tu, mwenye nywele za kipilipili, namna *hiyo*, vishungi saba vidogo vikining’inia mgongoni mwake. Na hawa hapa Wafilisti elfu moja wanakuja wakimzunguka.

142 Akatazama. Hakuwa mpiganaji hodari wa upanga. Hakuwa na Shahada ya Sanaa, wala Ph.D., wala LL.D. kujua jinsi ya kushughulikia hali hiyo ya mambo. Lakini alijisikia huku nyuma, angali alikuwa na ile ahadi. Ndipo akashawishika. Hakuwa na mafunzo, alishawishika ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye, maana alikuwa na ule ushahidi ukining’inia kote kumzunguka.

143 Ee Mungu. Laiti ningeweza kufanya jambo. Laiti ningeweza . . . nilikuwa nayo kwenye ndoo, ningeweza kuimwaga chini ya shingo ya kila mtu, na kusema, “Ijaze. Hii hapa. Ijaze.” Huh? Loo, naam.

144 Kushawishika kisha kuhusika juu ya watu wake. Musa, nabii mtoro, alikuwa amepoteza matumaini yote. “Loo, Israeli haitakombolewa kamwe. Hilo lilikuwa ni jambo ambalo mama aliniambia.” Lakini alijaribu kulifanya mwenyewe. Hivyo ndivyo kanisa linavyojaribu kufanya, kujaribu kufanya Waumoja wote kuwa Wautatu, Wautatu kuwa Waumoja, Church of God liwe *Ninii*, na Wamethodisti wawe Wabaptisti. Hutafanya hivyo kamwe. Unafanya nini? Ni sa—saikolojia yake tu, mabadiliko ya nia. Kuna nini kwenye lundo hilo lote, ambapo unamwona Mungu katika jambo hilo lote?

145 Hiyo ndiyo sababu. Hiyo ndiyo sababu hata wao hawajashawishika. Wameshawishika kwamba wao ni dhehebu, bali hawajashawishika kuwa Mungu yu pamoja nao, la sivyo hawangekuwa wakifanya jinsi wangefanya. Wanasema wameshawishika, lakini maneno yao. . .matendo yao yanaongea kwa sauti kubwa kuliko maneno. Kwa matunda yao mnawatambua, kama maungamo yao ni ya kweli au la. Wakisema wanamwamini Mungu, ya kwamba Yeye ni Mungu mkuu, Yeye ni Mungu yeye yule, na kukana Neno Lake. Loo, jamani! Wanasema lilikuwa kwa ajili ya siku nyingine. Ni upuuzi.

146 Musa, alihitaji kushawishika. Hakuwa na ujuzi, hata hivyo alikuwa—alikuwa mtu mashuhuri. Alikuwa askari wa vita. Alifikiri kwa mafunzo hayo aliyokuwa nayo, alimwua Mmisri, akarusha mavumbi juu yake, akasema, “Nitafanya hivyo.” Ndipo jaribio dogo la kwanza lilipokuja, “Siku za miujiza lazima zimepita.” Ndipo huyo akaenda nyikani.

147 Lakini siku moja Mungu akamshika nabii huyo mtoro. Aliona kichaka kikiwaka moto. Akasema, “Nilisimama na kukitazama kwa muda, hakikuteketea.” Akakikaribia, akasema, “Hicho ni kichaka cha ajabu. Ninashangaa ni kemikali za aina gani zimepakwa kwenye majani hayo, zinazoendelea tu kuwaka moto.”

Hiyo Sauti ikasema, “Musa, vua viatu vyako.”

“Naam, Bwana.” Huyu hapa anakuja.

148 Kasema, “Kwa nini kupoteza umakini? Nimesikia kuugua kwa watu Wangu. Uliwakimbia kwa nini? Kwa nini uliukwepa wajibu wako? Nimesikia kuugua kwa watu Wangu. Ninakumbuka Neno Langu nililomwahidi Ibrahimu baba yao.”

149 Tunahitaji Musa mwingine. Musa alishawishika kabisa. Alishawishika sana mpaka kesho yake akamweka mkewe juu ya nyumbu, na mtoto nyongani mwake, naye huyu hapa akishuka kwenda Misri kwa ajili ya uvamizi wa mtu mmoja. Mnajua, unaposhawishika inakufanya utende kigeni kwa ulimwengu. Lakini unaposhawishika, umeshawishika. Kasema, “Unaenda wapi, Musa?”

“Ninashuka kwenda kuiteka.” Naye akaiteka. Kwa nini? Alishawishika kwamba huyo alikuwa ni Mungu.

150 Hiyo ndiyo shida yetu sisi Wapentekoste. Baraka hii tuliyo nayo, wakati mwingine tunashangaa. Hiyo—hiyo ni kweli, jamani. Kamwe sijaribu, kusema uwongo sasa. Hiyo ni kweli. Matendo yetu yanathibitisha hilo.

Simama Musa. Kasema, “Musa, hebu—hebu kidogo. Ninaamini ulikosea, bwana. Mimi ni daktari wa uungu.”

“Simile.” Alishawishika kabisa. Na ndipo aliposhawishika, basi akahusika na yale ambayo Mungu alitaka yafanywe.

151 Nami nimeshawishika leo kwamba ninajaribu niwezavyo kufanya kile ninachofikiri Mungu anataka kifanywe, ni kuukatakata wakati huu wa kanisa la Laodikia. Nilisimama peke yangu pamoja na Mungu, lakini nimejaribu kutimiza agizo langu. Sijayachanganya. Nimejaribu kuwaambia pande zote mbili, na kujaribu kuvuta kutoka kwa kila upande, si kujiunga na yeyote kati yao, kwa sababu nimeshawishika, na ninahusika. Ninaliona papa hapa katika Biblia. Nisingethubutu kukusomea, lakini na—najua hilo. Nyote mnajua hilo wenyewe.

152 Sasa, angalieni, kushawishika, halafu kuhusika. Naye Musa alihusika aliposikia Sauti ya Mungu ikinena naye, naye alijua ilikuwa ni ya Kimaandiko. Wakati mtu amesimama pale akiangalia kichaka hiki kinachowaka moto, na kusikia Sauti ya kimbinguni ikimwita, na kumwagiza asimame papa hapa pamoja na Maandiko, alishawishika kabisa.

153 Basi tunapomwona Mungu akiahidi jambo lolote, unaliona likitendeka namna hii, unasema, “Naam, labda ilikuwa hivyo. Sijui sasa. Labda Utatu ni sahihi. Labda wa Umoja, labda Wamethodisti wako sahihi.” Hujashawishika bado. Hiyo ni kweli. Hujashawishika. Huna budi kushawishika, ndipo unahusika.

Kesho yake alikuwa akienda zake kazini, akishuka kwenda Misri kuiteka.

154 Wale wana wa Kiebrania huko Babeli, wa—walishawishika ya kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kuwakomboa. Sasa, sikilizeni kwa makini sana. Walishawishika kwamba Mungu angeweza kuwakomboa, ndipo wakachukua msimamo wao.

Sasa mnaona ninachojaribu kuwafanya mfanye?

155 Walijua ya kwamba Yeye alikuwa amewawekea ahadi ya kutoisujudia sanamu, kwamba Yeye alikuwa “Bwana, Mungu wako,” nao hawangeweza kuisujudia sanamu. Walishawishika kwamba hilo lilikuwa ni Neno la Mungu. Walishawishika kwamba Yeye angeweza, kama Ibrahimu, kutimiza kile alichoahidi. Na basi kama walikuwa wameshawishika kwa Neno la Mungu, Mungu alihusika kulihusu. Whiu!

156 Mnajua ninamaanisha nini? Rudini kwenye Neno. Chukueni maagizo hayo niliyowaambia, hivi majuzi usiku. Kama umeshawishika ya kwamba hilo ni Neno la Mungu, kama umeshawishika na unajua Yeye anaweza kulifanya tena, Yeye ana uwezo wa kutuletea Mtaa mwingine wa Azusa, kama umeshawishika kwamba ni kweli kuhusu Neno Lake, basi Mungu anajali kuhusu Neno Lake kutimizwa. Lakini bado hatujashawishika. Hiyo ni kweli. Hatujashawishika. Kama tungeshawishika, jambo fulani lingetukia.

157 Unasema. . .Hili—hili—hili hapa lengo lako. Una bunduki yako, lakini hama imeshushwa. Vuta, vuta, vuta; lakini hama imeshushwa. Shawishika, vuta hama nyuma, na kisha uiguse. Jambo fulani linatendeka. Kuna moto unaoshuka. Unaona, bado hatujashawishika.

158 Waliposhawishika ya kwamba Yeye alikuwa anaweza kusimama na Neno Lake, Naye akaishi, Naye angethibitisha Neno Lake, basi walihusika. Ndivyo ilivyo sasa, ambapo kama tumeshawishika Yeye hulitimiza Neno Lake, kama tumeshawishika kwamba Mungu hutimiza Neno Lake, Mungu anahusika kulitimiza Neno Lake ndani yetu kama tunalijali.

159 Martha alishawishika alipokimbia kule nje, na kusema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa." Tazama. Baada ya Yeye kumkatalia, alikuwa kama maskini yule mwanamke wa Kiyunani: kung'ang'ania. Hatung'ang'anii vya kutosha, kwa sababu hatujashawishika vya kutosha.

Asanteni kwa subira yenu, lakini ngojeni kidogo tu, hadi nimalize.

160 Alishawishika. Haidhuru alifanya nini, na kile mtu mwingine yeyote alichosema juu Yake, alishawishika kwamba Maandiko yalikuwa yamemtambulisha ipasavyo kuwa Mwana wa Mungu. Na kama alikuwa Mwana wa Mungu, Mungu akitenda kazi kupitia wanadamu. . .

161 Ikiwa yule mwanamke huko nyuma katika Biblia, Mshunami, angeweza kumpokea mtoto wake kwa sababu Mungu alikuwa. . .alimtambulisha mtu huyo kikamilifu kuwa nabii, Eliya, na kama alikuwa ndani ya nabii Wake, vipi kuhusu Mwanawe? Naye Mwanawe alikuwa ni Mungu-nabii. Kwa hiyo basi alishawishika kwamba hiyo ilikuwa ni kweli. Labda alipokuwa akitengeneza biskuti na kukaanga mayai, alikuwa akiwazia hayo wakati dada yake alipojaribu kumkemea.

162 Angalieni. Sasa, wazieni jambo hilo. Alitoka mbio, akasema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini nimeshawishika kabisa, nimeshawishika kabisa hata sasa, kama ukimwomba Mungu, Mungu atakupa kile unachoomba."

163 Loo, ndugu, kama tungeweza kumkubali huyo Roho Mtakatifu ambaye yuko papa hapa miongoni mwetu sasa hivi

kwa njia hiyo, kushawishika kabisa, kushawishika kabisa. Kwa nini? Alikuwa amemwona akijitambulisha Mwenyewe (mwanamke wa mwana wa Naini), naye alijua ilikuwa hivyo. Aliliamini, hata hivyo Yeye alikuwa mwanadamu. Hata hivyo, aliamini.

164 Haikuwa ni Yeye sana; ilikuwa ni Mungu. Alikuwa Mungu-mtu. Alijua kwamba alistahili katika Maandiko. Alikuwa Masihi. Mungu alikuwa amethibitisha jambo hilo na kulithibitisha kwa Neno Lake. Na kama—kama alivyosema, "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi. Si Mimi. Ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu. Anatenda kazi. Sifanyi lolote mpaka nimwone akilifanya kwanza." Mnaona?

165 Alishawishika, naye akasema, "Bwana, ingawa amekufa, ingawa amezikwa, ingawa ananuka, lakini hata sasa, ukimwomba Mungu, Mungu atakupa."

166 Akajiinua Mwenyewe, na kumpa ukweli ambao haukuwa umewahi kusemwa juu Yake hapo kabla: "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima." Mnaona, alikuwa amefikia kiwango fulani wakati huo. Angeweza kuendelea pamoja naye. Na wakati kanisa linapofikia kiwango fulani, utasonga mbele.

167 Kama nilivyosema kuhusu wanawake. . . Yule mtu aliyeniambia, alisema, "Achana na hao wanawake kuhusu nywele zao na mambo kama hayo, na wanaume hawa kuhusu madhehebu yao, na kadhalika." Kisha akasema, "Kwa nini wewe—kwa nini usiwafundishe jinsi ya kupokea karama? Watu wanaamini wewe ni nabii."

Nikasema, "Sidai kuwa hivyo."

168 Kasema, "Lakini watu wanafikiri ndivyo ulivyo." Kasema, "Wanaamini hilo." Kasema, "Ninaamini, mimi mwenyewe." Kasema, "Kwa nini usiwafundishe jinsi ya kupata vitu vya kumsaidia Mungu?"

Nikasema, "Ngojea mpaka watakapojifunza abc zao; ndipo tutawafundisha aljebra." Hiyo ni kweli.

Na wakati utakapolikubali! Martha, "Ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu ambaye alikuwa aje ulimwenguni."

169 Kasema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima." Loo, angeweza . . . Akapata ufunuo wakati huo. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo atakuwa anaishi. Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa hata milele. Je, unasadiki haya?"

Akasema, "Ndiyo, Bwana." Loo, jamani!

"Mmemzika wapi?" Alishawishika kwamba Yeye angeweza kufanya jambo hilo.

170 Yairo alishawishika kama Yesu angeweka mikono Yake juu ya binti yake mgonjwa kwamba angepata afya, haidhuru kanisa lake lilisema nini juu yake. "Msichana wangu mdogo

sasa yuko karibu na kufa. Njoo tu, uweke mikono Yako juu yake. Nimeshawishika." Kidogo alikuwa ni mwaminio wa kisiri. "Weka mikono Yako juu yake, naye ataishi."

Ndipo ujumbe ukaja, "Amekufa." Moyo wake ukaanza kuruka.

171 Yesu alikuwa njiani, kasema, "Je, sikukwambia, kama ukiamini tu, utaona utukufu wa Mungu?" Alishawishika. "Hebu tuendelee kutembea," alishawishika kabisa.

172 Yule askari wa Kirumi, kwa kuwa ni M—Mrumi, alitambua ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu. "Nimeshawishika kwamba Wewe una uwezo juu ya kila ibilisi. Nimeshawishika kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Sistahili Wewe kuja chini ya paa langu. Lakini laiti ningaliweza tu kukusikia ukinena Neno nimeshawishika mtumishi wangu angeishi." Amina.

173 Mungu turehemu. Kama mpagani angeweza kutarajia hilo, na kushawishika kabisa juu ya kile alichokiona Umasihi wa Yesu ukithibitisha, naye akiwa ni mpagani wa Kirumi, vipi kuhusu kanisa, kanisa la Kipentekoste ambalo limekuwa na miaka hamsini ya kufanya kazi na bado halijashawishika? Miaka hamsini huko Louisiana, kumwagika baada ya kumwagika, na bado. . .

174 Yule askari wa Kirumi, mpagani, alisema, "Nena tu Neno. Hayo tu ndiyo ninayotaka kujua, ni yale Neno lisemayo." Ninakupa maagizo. Hivyo ndivyo Neno lilivyosema. Je, umeshawishika? Yule Mrumi alihusika juu ya mwanawe, na alishawishika kama angeweza kumfanya Yesu aseme Neno, nalo lingeweza kuwa ni Neno la Mungu, lililofanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Alishawishika.

175 Yule mwanamke aliyekuwa anatokwa damu, ingawa hakuna mtu aliyewahi kufanya hivyo, lakini alishawishika kabisa kwamba akigusa upindo wa vazi Lake, angepona. Ilibidi aondoke nyumbani kwake, akiwa dhaifu. Jinsi ningeweza kulielezea kwa muda kidogo, nishuke niende kupitia kwa Brigham Young, na hao wengine wote, moja kwa moja kupitia kwa hao watu, "siku za miujiza zimepita." Angeweza kupanda katikati ya miguu yao, na kujipenyeza kati yao, maskini mwili wake, mdogo, dhaifu. Naye alishawishika kabisa. "Nikiweza tu. . .Hata huna haja ya kuongea nami. Kama kwa njia fulani naweza tu kupata mguso kutoka Kwake, kutokwa kwangu na damu kutakoma." Alishawishika.

176 Yule mwanamke kisimani alishawishika Yeye alikuwa ndiye Masihi hapo alipoona ishara hiyo ya Kimaandiko. Kasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii." Sasa, tunafunga. "Naona ya kuwa Wewe ni nabii."

Alijua. . .Alimwambia, kasema, "Nenda kamwite mumeo."

Akasema, "Sina yeyote."

Kasema, “Una watano.”

177 Akasema, “Bwana, najua, nimeshawishika kabisa ya kwamba Wewe ni nabii. Lakini tumefundishwa. . .Hatujakuwa na manabii kwa mamia ya miaka, nami najua ya kwamba Wewe ni nabii. Sasa, nitajua kitu fulani. Tunajua ya kwamba, kadiri tunavyoweza kuona katika Maandiko, anayefuata ni Masihi. Na ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya. Sasa, kama Wewe ni nabii, utaniambia kweli, kwa sababu Neno la Bwana humjia nabii. Nami ninakuona ukifanya ishara. Ni ishara ya ajabu. Masihi atafanya ishara hiyo.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

178 Alishawishika. Hakumhoji tena. Angalieni. Moja kwa moja akaweka chini mtungi wa maji, naye alihusika kwamba mtu mwingine alijua jambo hilo. Amina. Alishawishika. Nini? Aliona ishara ya Kimaandiko. Naye akamsikia Mtu huyo Ambaye alimjua kuwa nabii, nalo Neno liko pamoja na nabii, naye alijua ilikuwa ni kweli, ya kwamba Yeye asingemwambia uongo. Naye. . .alishawishika ya kwamba Yeye alikuwa nabii, naye akaiona hiyo ishara ya Kimasihi. Na wakati alipomwambia ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, hiyo ilitosha. Alishawishika, naye akahusika kuhusu watu wake. Akakimbia mtaani akisema, “Njoni, mwone Mtu. Mtu huyo aliniambia yale nimekuwa nikifanya. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi?” Alishawishika. Hakika.

179 Petro alishawishika, akiketi kwenye kipande hicho kinene wakati alipokuja na Andrea, naye Yesu akamwambia, “Simoni, baba yako, Yona.” Akashawishika. Hilo lilikuwa halijafanyika tangu yule nabii wa mwisho. Alishawishika ya kwamba Huyo alikuwa Ndiye.

180 Filipo akasimama na kuangalia hilo. “Jamani, ajabu.” Alishawishika. Aliposhawishika, akahusika. Alikuwa na ndugu huko juu aliyeitwa Nathanaeli. Walikuwa wamesoma Maandiko pamoja. Alihusika kuhusu Nathanaeli kujua jambo fulani juu yake.

Tuangalieni siku hizi. Kwa sababu halijaundiwa dhehebu, au kufanyiwa makundi, au kung’arishwa jinsi tunavyotaka, bado hatujashawishika.

Thibitisho ni Neno la Mungu.

181 Filipo, mshiriki wa kanisa pia, lakini alishawishika, halafu akahusika juu ya ndugu yake, kwa hivyo akakimbia huko na kumwambia, “Njoo, umwone Yule tuliyempata: Masihi.” Naye akaanza kuzungumza na Filipo wakienda, ama, ilikuwa ni Nathanaeli, wakitembea barabarani, naye Nathanaeli alitaka kujionea jambo hilo. Kwa hivyo akaja mkutanoni. Ndipo alipokuja mkutanoni na kuliona likifanyika, alishawishika kabisa. Lakini sisi hatujashawishika. La, la.

182 Mwenendo wa Kipentekoste wa siku hizi bado haujashawishika. La. Ungelishawishika, wangehusika. Umerudi katika kiwango cha Kifarisayo: umeunda madhehebu, haujashawishika. Ikiwa umeshawishika kabisa, ungehusika. Hao Mafarisayo, waliweza kuona na kujua ya kwamba hiyo ilikuwa ni kweli, lakini hawakushawishika kabisa kwa sababu walimu wao waliwafundisha kukaa mbali nayo. Na hiyo ndiyo shida siku hizi, ni, Mafarisayo wengi kupita kiasi, walimu, shirika likijaribu kuwafukuza watu, kwa sababu hawajajiundia dhehebu. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini wale walio na moyo mmoja wanaliona.

183 Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Nitaingiza wazo dogo hapa nanyi mtafikiri ni Baptisti, lakini sivyo, ni Biblia. Angalieni. Kulikuwa na hao wasomi waliofunzwa vyema, walioiangalia ile ishara aliyoifanya, na kumwita ibilisi. Lakini huyu hapa kahaba, lakini *ndani* yake, mlikaa hiyo mbegu ya Mungu iliyochaguliwa tangu asili. Hakuwa amewahi kuona kitu kama hicho. Na mara hiyo Nuru ilipoigusa ile mbegu, Uhai ukachipuka. Kwa nini? Kwanza kabisa ilikuwa na Uzima ndani yake.

184 Ni majira ya kupukutika mwakani, mbegu hufa na kurudi kwenye udongo. Lakini hebu hilo jua liipige tu. Ikiwa chembe ya uhai ipo, itachipuka. Mwanamke huyu katika hali yake ya kutisha ali-. . .alikuwa amechaguliwa tangu zamani. Jina lake liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu. Ndipo alipoona hiyo Nuru ya Mungu ikichipuka, hakuna kitu kingaliweza kumshikilia, ilichipuka ikawa Hai.

Wakati makuhani wenye elimu, wao walisema, "Vema, hu—hu—huyo ni baba mtakatifu *nanii*."

Sijali ilikuwa ni nini. Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi na kazi zake mnazifanya."

Yule kahaba akasema, "Hapana shaka wewe ndiwe Masihi."

Ndipo alipomwambia alikuwa ndiye, akashawishika. Ati nini? Ile mbegu iliyochaguliwa tangu zamani, nuru ilipoangaza kwa mara ya kwanza, aliitambua.

185 Na siku hizi, tunapoenda (kunradhi usemi huu), nami ninaona hiyo kazi ya Mungu, Roho Mtakatifu akishuka na kuanza kudhihirisha jambo fulani, mbegu iliyochaguliwa tangu zamani inakaa pale, inainyakua. Usingeweza kuipindua kutoka kwake kwa chochote kile.

Hao wengine watakwenda zao na kusema, "Unashangaa ni ujanja wa aina gani? Hapana shaka pana namna fulani ya udanganyifu kwake mahali fulani."

Lakini hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu zamani haiulizi maswali. Imeshawishika kabisa kwamba ni Mungu anayetembea kulingana na ahadi Yake katika Biblia.

186 Tunapaswa kuwa mbele zaidi kidogo barabarani, hasa, kuliko Mtaa wa Azusa. Kanisa linapaswa kuwa *hapa* juu. Hapa lilianza kwa kuomboleza, na kulia, na kumjia Mungu. Nalo limeanguka mbali sana, na hiki hapa kitu fulani *hapa* juu ambacho kanisa linapaswa kuwa nacho kukabiliana nacho. Mnaona? Lakini hata hivyo wao—wao hawajashawishika. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu halihusiki. Hiyo ni kweli.

Nathanaeli alipoona jambo hilo, alishawishika.

Ninafunga sasa hivi. Ninayo mengine kadhaa hapa ninayotaka, kuzungumzia, lakini nitazungumza kuhusu mimi na wewe kwa dakika chache.

187 Vipi kuhusu sisi? Hapa tunasherehekea mwaka wa hamsini wa Pentekoste huku Louisiana. Na kwa kweli, ishara ambazo kamwe hazikutokea mwanzoni ni kubwa kuliko zile. . .ni kubwa zaidi sasa. Huko kulikuwa ni kutayarishwa kwa shamba lisilopandwa mbegu, kujiandaa kwa ajili ya ukweli halisi utakaopandwa ndani yake. Na wakati mtu fulani alipokuja akipanda mbegu, mlijiundia dhehebu na kuzika kitu hicho kabisa. Uigaji wa kimwili ulikuja kuiga.

188 Hivi hamjui hiyo ni kazi ya ibilisi kujaribu kuyapofusha macho yenu? Je, hamjui kulikuwa na akina Yesu wa uongo walioinuka kabla ya Kristo wa kweli kuja? Ni kuondoa tu. Ni ibilisi akijaribu kuondoa jambo hilo. Hilo ndilo jambo lile lile ambalo limekuwako siku hizi, kujaribu kukuondolea mbali. Watu wenye mifano mibaya, na kanuni za imani, na kadhalika, wakijaribu kuiga, wanawezaje kufanya jambo hilo? Biblia ilisema wangefanya hivyo, kama vile Yambre na Yane walivyompinga Musa. Lakini kasema, “Upumbavu wao utadhihirika.”

189 Musa alikuwa na jambo moja la kufanya: kusimama mkweli kwa agizo lake. Ndipo hatimaye wakati ukafika ambapo walitupa fimbo zao chini na kujaribu kufanya jambo lile lile. Ndipo fimbo ya Musa ikawameza. Um-hum. Je, umewahi kuwazia hizo fimbo zilienda wapi? Uh-huh. Hum. Vema.

190 Kushawishika: tunaposhawishika, basi tutahusika. Lakini tutakuja, nao mkutano utaendelea, naye Kristo atashuka, na kuthibitishwa kwa Neno, na kufanya jambo lile lile alilofanya; ikionyesha ya kwamba ni siku ambayo kanisa halina budi kukatwa vipande vipande maana limemtupa Kristo nje, wakaunda dhehebu wakamtupa kutoka miongoni mwao namna hiyo, wakimtoa kwao namna hiyo, akasimama nje, bado anabisha.

191 Sasa, ilionekana kana kwamba angetoka nje, angeondoka tu aende zake. Lakini sivyo, Yeye angali amesimama, akibisha,

kama alivyokuwa katika siku za Nuhu, uvumilivu, hataki mtu yeyote apotee, bali wote waifikilie toba: amesimama, akibisha, kusikiliza kama Yeye anaweza kusikia, je, utamkaribisha? La, hakuupata.

192 Kisha akasema, "Nitakutapika kutoka kinywani Mwangu." Kweli. Nawe unaona kukatwa kwa Neno na Roho. Unamwona Roho Mtakatifu akishuka na kufanya mambo ambayo hayajapata kujulikana tangu siku za Bwana Yesu Kristo na wanafunzi Wake. Nasi tutaketi, na kuliangalia na kuondoka. Je, kweli tumeshawishika, au ni mikate na samaki?

193 Yesu aliwalisha. Ni nani angeweza kuumba mkate, isipokuwa Mungu? Mungu yeye yule aliyeleta mkate kutoka angani, na kuimiminia kule, hawa hapa Waebrania wamesimama pale, wakamtazama Yeye akiumega mkate huo na kuwagawia namna hiyo, akizidisha ile mikate. Mwokaji yeye yule aliyeioka Mbinguni alikuwa akiioka papa hapa duniani, na kuwapa. Kweli. Nao wakasema, "Hiyo ni ajabu. Loo, nimeshiba kabisa sasa, Bwana. Loo, huo ulikuwa mkutano mkuu."

194 Yesu akasema, "Lakini ngojeni kidogo. Nina jambo la kuwaambia: Punje ya ngano isipoanguka ardhini . . . " Mahubiri haya yote, akaanza kuhubiri, na kuwarudisha kwenye Neno.

Kasema, "Aaaw, hiyo—hiyo ni ngumu sana kuelewa. Hatuitaki hiyo tena." Wakaanza, kuondoka.

Na baadhi ya makasisi Wake wakasema, "Sasa, ni nani tungeweza kumfanya aamini kitu kama hicho? Tutaondoka pia."

Alisimama tu na kuwaangalia.

Hao kumi na wawili, kundi dogo aminifu, kama kifaranga akisimama karibu na mama yake, Yeye aligeuka, akasema, "Mnataka kwenda, pia?"

Petro akasema, "Twende wapi, Bwana?" Mnaona?

195 Hivi Yeye hakuwaambia, ya kwamba, "Niliwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu"? Hiyo ndiyo Nuru iliyoangazia mbegu hiyo. Hakuna njia ya kuiondoa. Ni Uzima wa Milele. "Nitampa Uzima wa Milele na nitamfufua siku ya mwisho. Wote aliowajua tangu zamani amewaita; wote aliowaita amewahesabia haki; wote aliowahesabia haki tayari amewatukuza. Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu isipokuwa Baba Yangu amwite, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu."

"Kwa nini unahubiri basi, Ndugu Branham?"

196 Sijui ni akina nani; Yeye anawajua. Kazi yangu ni kupanda Mbegu. Sijui zinaangukia wapi, lakini ninazipanda tu. Mungu anathibitisha. Popote inapoangukia, na kugonga namna *hiyo*, upesi inakuwa Hai ikiwa kwenye udongo mzuri. Ikiwa kwenye mwamba, siwezi kuisaidia. Msingi fulani wa kimadhehebu, siwezi kuisaidia. Jambo pekee, nitaendelea tu kupanda Mbegu. Najua Yeye yuaja. Ninaamini. Nataka kuishia hilo.

Nimeshawishika kwamba anakuja. Nimeshawishika kwamba anakuja hivi karibuni. Nimeshawishika.

197 Neno moja zaidi, tafadhalini. Yesu alishawishika kwamba angefufuka siku ya tatu. Mwangalieni. Andiko moja tu katika Biblia la kuliunga mkono jambo hilo, na hilo lilikuwa ni la mtu ambaye hatimaye alirudi nyuma. Lakini Daudi katika Roho . . .

Siku moja alisema, "Mnaonaje juu ya Kristo? Yeye ni Mwana wa nani?"

Nao wakasema, "Yeye ni mwana wa Daudi."

198 Akasema, "Basi kwa nini—kwa nini Daudi . . . " sasa, ondoa sehemu ya mwili, " . . . kwa nini Daudi, katika Roho, akamwita Bwana, akisema, 'BWANA alimwambia Bwana wangu, keti mkono Wangu wa kuume?'"

Katika Ufunuo alisema, "Mimi ni Shina na Mzao wa Daudi. Nilikuwa kabla yake; mimi ndiye; na mimi—mimi niko sasa."

199 Tangu wakati huo hawakumwuliza chochote. Hicho kilikuwa ni kitendawili kwelikweli. Hawakuelewa hilo. Mafunzo yao ya kitheolojia hayakuwa yamewafikisha hapo. Wala hayawezi bado. Um-hum. Wamejaribu kwa muda mrefu wala hawawezi kulielezea bado. Linafunuliwa tu kwa wale ambao litafunuliwa.

200 Yesu alishawishika kabisa. Alisema . . . alitokea mbele yao, akasema, "Liharibuni hekalu hili, nitalisimamisha katika siku tatu. Liharibuni, fanyeni chochote mnachotaka kulifanyia. Nitaliinua tena baada ya siku tatu." Whiu! Kwa nini? Alishawishika kabisa. Alijua Yeye alikuwa ni Nani. Alijua kile Mungu alikuwa ameahidi.

201 Loo, kama, kwa mfano, ikiwa tungeweza kusoma jina letu ndani Yake: "Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa; kwa ahadi Yake nimeokolewa; kwa Damu Yake mimi ni sehemu Yake; kwa ahadi Yake nitafufuka tena katika siku za mwisho." Hmm?

202 Alijua ya kwamba alisomwa moja kwa moja katika Maandiko. Alijua mahali Pake. Hakuna mtu aliyepaswa kumwambia chochote kuhusu hilo, ingawa ha—hakuzunguka akijigamba kuhusu hilo. Hiyo ilionyesha—hiyo ilionyesha kile alichokuwa.

203 Yohana hakuzunguka akijigamba juu ya kile alichokuwa, kifua chake kimetokeza, "Mimi ni Dk. *Nanii*, nina *hiki-na-hiki*." La, la. Yohana alijitokeza tu kama mtu wa kawaida. Vivyo hivyo na Yesu. Kazi zao zilishuhudia kile walichokuwa. Hiyo ni kweli. Kazi zao zilifanya hivyo. Kwa hiyo Yeye hakufanya hivyo. Alizunguka tu, akasema . . .

Walisema, "Tunapaswa kumnyonga. Tunapaswa kumwondosha katikati yetu."

Akasema, “Liharibuni hekalu hili, nami nitalisimamisha tena, siku ya tatu.” Uh-huh.

Mbona, alijua Daudi alisema, “Sitaiacha nafsi Yake kuzimu; wala sitamwacha mtakatifu Wangu, aone uharibifu.”

204 Nanyi watu mnawezaje kuamini, ama mtu yeyote aamini . . .? Kanisa Katoliki linawezaje kuamini . . .? Wengi wetu, kuzaliwa pasipo na dhambi ya asili, tunaamini hivyo, lakini inapofikia . . . Tunajua ya kwamba ile chembe ya Damu ilitoka kwa Mungu. Tunajua Mungu aliumba chembe hiyo ya Damu iliyosababisha kuzaliwa na bikira. Si chembe ya Damu tu bali aliumba yai la mwanamke pia, maana hakuna mwenye mwili aliye mtakatifu. Ikiwa hilo lingekuwa yai kutoka kwa Mariamu, basi ingebidi awe na namna fulani ya m—msisimko ili kulishusha hilo yai. Lakini hakujua lolote juu yake. Roho Mtakatifu tu ndiye aliyemfunika. Kama ulifanya hivyo, unaona kile ambacho ungemweka Mungu kumfanyia mwanamke?

Utukufu. Yeye alikuwa ni Mungu. “Sitamwacha mtakatifu Wangu, mwili Wake . . . ” Je, ingewezaje kuwa takatifu kupitia tamaa ya kujuana kimwili? Naam, kama ni hivyo, sisi sote ni watakatifu.

205 Hakuna watu watakatifu. Hakuna mlima mtakatifu, hakuna kanisa takatifu. Ni Roho Mtakatifu, Mungu mtakatifu katika Kanisa, juu ya mlima. Si watu watakatifu; Mungu mtakatifu ndani ya watu. Mwili huo ulikuwa ni wa Mungu, Mungu Mwumba.

206 Yesu alihusika. Alijua jambo hilo, na kushawishika ya kwamba angeufufua siku ya mwisho, kulingana na ahadi ya Maandiko. Ninafunga kwa kusema hivi, muda unaenda sana, hebu niseme jambo hili moja kisha nitaondoka: nimeshawishika kabisa kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nimeshawishika kabisa ya kwamba Hiki tunachonena habari zake na kukiona hapa ndani ni Roho Mtakatifu. Nimeshawishika kabisa.

207 Mtu alisema hivi majuzi, alisema, ama, ilikuwa ni msichana mdogo, nilikuwa nikizungumza naye, akasema . . . nikasema . . . Alizoea kutoka pale nje, akiwa amevalia kama kila kitu, nami nilikuwa nikizungumza naye. Alikuwa na watu ambao walienda kwenye kanisa lingine, walidhaniwa kuwa ni Wakristo. Nikasema, “Hivi hujionei aibu?”

208 Yeye ni, “Aah,” kasema, “Bw. Branham . . . ” Akitafuna chingamu yake namna *hiyo*, naye alionekana kama kitu fulani kutoka Afrika. Huenda angekuwa msichana mrembo, kama angekuwa amevalia kama binadamu. Naye akasimama pale, akasema, “Bw. Branham, bila shaka, hapo, unaona, wewe ni mtu mwenye umri wa makamo. Hakika. Huwezi kuamini, lakini sisi ni watoto.”

209 Nikasema, "Angalia hapa. Wakati sikuwa na umri wako, bado nilikuwa nimeshawishika kwamba Hii ni kweli. Nilitumia maisha yangu yote juu Yake. Laiti ningekuwa na maisha milioni moja ya kutumia Kwake."

210 Nimeshawishika kabisa kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Nimeshawishika kabisa kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nimeshawishika kabisa kwamba yule Malaika aliyeshuka ambaye niliwazungumzia juu yake, kabla hajaja, Yeye aliithibitisha, na kusema ilikuwa kweli, na amethibitisha kuwa ni kweli.

211 Nimeshawishika kabisa kwamba ule uvuli wa mauti ambao nimekuwa nikiwaambia watu, na kuuona huo kule, kamera za kisayansi na kadhalika zimeyathibitisha mambo haya. Nimeshawishika kabisa kwamba Ujumbe wangu unatoka kwa Mungu. Nimeshawishika kabisa kuwa sio akili yangu ya kimwili iliyojivuna. Ni Neno la Mungu.

212 Nimeshawishika kabisa, nimeshawishika kikamilifu, ya kwamba ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Nimeshawishika kabisa kwamba Yeye yuko papa hapa sasa. Nimeshawishika kabisa kwamba amepiga kambi hapa ndani. Nimeshawishika kabisa kwamba atajibu maombi yetu, ikiwa tutahusika, kushawishika, na kuyafungua maisha yetu Kwake. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

213 Bwana, huu mkutano mkubwa uko karibu tu kufungwa. Tumekuona ukitenda kazi, Bwana. Loo, tumekuona wakati wote. Tumekuona miaka hii yote. Tunakuona Wewe ukiwa na nguvu zaidi, kanisa likizidi kudhoofika. Bwana, yachukue maneno haya machache, sivyo, Bwana? Si—siwezi kufanya mengine nayo, Baba.

214 Lakini, loo, nina hakika, Bwana, kama walishawishika, kama kila mtu angeshawishika, kusingeweza kuwa na utulivu popote. Kama maskini ndugu yetu wa thamani . . . Ulipomwaga Roho Wako kwa mara ya kwanza katika mfano wa ubatizo kabla ofisi hizi kuu hazijaingizwa . . . Maana ni wakati sasa. Adui anakuja kama mafuriko. Unainua kiwango dhidi yake.

215 Bwana, ninawaombea. Jalia maneno haya machache asubuhi ya leo yaanguke juu ya mioyo ya watu. Jalia yasianguke penye mawe. Jalia yaanguke kwenye udongo mzuri, nayo Nuru ya Uzima wa Milele iangaze juu ya hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani. Nina hakika itafanya hivyo, Bwana. Uliahidi, na ukasema tufanye jambo hili, Nawe ungeshughulikia mengine yote. Na nina hakika itafanya hivyo.

216 Kwa hiyo ninayakabidhi Kwako, nalikabidhi kusanyiko hili Kwako. Ninajiweka miongoni mwao kama Musa alivyofanya watu wake. Bwana, mimi ni mmoja wa watu hawa. Mungu, nimejaribu niwezavyo kuwa mwaminifu. Unanishuhudia.

Nimesema kweli, na Wewe ni shahidi wangu kwa kuithibitisha. Nimesema kweli.

217 Ninawapenda watu hawa, Bwana, hawa Wapentekoste. Wengi wanaondoka, Bwana. Tofauti za kimadhehebu zinawaondoa. Ninampenda Mmethodisti huyu, Mbaptisti, chochote walicho. Ninawapenda, Bwana. Mimi ni mmoja wao. Tafadhali, Bwana, ninaombea kila nafsi. Ee Mungu, jalia Nuru iwashukie watu asubuhi ya leo, nao wapate kuiona.

218 Jalia kanda hii, inapoenda kote nchini, kote ulimwenguni, na ipate mahali pake pa kukaa. Ielekeze, Bwana, pale pale hizo Mbegu zilipo. Sijui ziko wapi. Lakini wakati kweli hii ya Injili, iliyothibitishwa na Mungu, itakapoiangukia, nina hakika itakuwa Hai.

Wao ni Wako, Baba. Ninajikabidhi pamoja nao Kwako kwa ajili ya kazi ya Injili katika siku za mwisho. Katika Jina la Yesu. Amina.

. . . njia, Bwana!
Kuwa na njia Yako Mwenyewe!
Wewe ndiwe Mfinyanzi;
Mimi towe.
Nifinyange na unifanye
Kulingana na mapenzi Yako,
Wakati ninaposubiri,
Nimejitolea na ni mtulivu.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu na tuliwazie hilo.

Kuwa na . . . Yako.

Je, umeshawishika? Loo, jamani. Roho Mtakatifu akitembea kama Nuru . . .

. . . Mfinyanzi;
Mimi ni towe Yako.
Nifinyange na unifanye
Kulingana na . . . (Si mapenzi yangu, Bwana, Yako.)
Wakati ninaposubiri,
Nimejitolea na ni mtulivu.

62-1125M Kushawishika Na Kisha Kuhusika
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org